# Nipashe

Jumanne Agosti 2, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581025 *

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,019,301,493/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




## Serikali yapiga 'stop' vipimo lumbesa

UKURASA 4



## FIRMINO HATAKI KUONDOKA LIVERPOOL

UKURASA 22



# Samia: Siangalii makundi

• **Aahidi** kubadili ma-DC, ma-DAS... • **Chalamila** apewa...

*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### JAMHURI YAOMBA KIBALI KESI MENO YA TEMBO ISIKILIZWE MFULULIZO

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kukutwa na vipande 660 vya meno ya tembo vyenye thamani ya Sh. bilioni...

UKURASA WA 7

### MGANGA ADAIWA KUMWOGESHA DAWA YA MAPENZI MWANAFUNZI KISHA KUMTOROSHA

MWANAFUNZI wa kidato cha pili Shule ya Sekondari Usule, Kata ya Usule, Halmashauri ya Shinyanga...



Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala walioapishwa pamoja na viongozi wa taasisi mbalimbali za serikali wakila kiapo cha maadili ya uongozi katika hafla ya uapisho iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Matumizi tiketi kielektroniki mabasi mikoani kizungumkuti

UKURASA 4

NYONGEZA YA MISHAHARA

## TUCTA kutoa tamko

UKURASA 2


**MICHEZO** M-BET YAONYESHA UKUBWA WA SIMBA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Rais mstaafu wa Tanzania, Jakaya Kikwete ambaye ni Kiongozi wa Timu ya Waangalizi wa Uchaguzi Mkuu wa Kenya kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC-EOM) akizungumza na waandishi wa habari jijini Nairobi, jana. **Habari kamili Uk. 19**. **PICHA: EAC**

# Samia asema uteuzi hauangalii makundi

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema hana makundi kwenye uteuzi wa viongozi mbalimbali, anachoangalia ni sifa, uwezo, uaminifu na uchapaji kazi wa Mtanzania pamoja na imani yake kwa anayeteuliwa kuwa atamsaidia kazi.

Ameahidi kuendelea kufanya uteuzi wa viongozi wa ngazi za chini kama wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri ili kuboresha utendaji kazi wa kuwatumikia Watanzania hasa kwenye ukusanyaji wa mapato.

Aliwaonya viongozi wanaozuia wananchi kusema kero za eneo lao wanapotembelewa na viongozi wakuu, kwa kukusanya mabango yao ili yasionekane.

Rais Samia aliyasema hayo jana baada ya kuwaapisha wakuu wa mikoa tisa na makatibu tawala wapya, Ikulu Dar es Salaam, ambao pia walikula kiapo cha uaminifu.

"Teuzi hizi huwa zinafanywa kwa kushirikiana na wasaidizi wangu, lakini mwamuzi wa mwisho mpaka jina linatoka ni mimi kwa sababu nimepewa mamlaka hayo na Katiba," alisema na kuongeza:

"Na mimi katika kufanya kazi hii huwa sina makundi. Ninafanya kwa kuangalia sifa, uwezo, 'loyalty' (utiifu) ya mtu ambaye ninaamini kwamba atanisaidia na atakwenda kuhudumia wananchi kwa hiyo anayechukia atanisamehe," alisema Rais Samia.

"Kwa hiyo, kama imefanyika vizuri au vibaya lawama nabeba mimi na kama kuna mtu ambaye hajaridhika na utezi huu ndio hivyo, wasaidizi wangu huwa wananisaidia tu kwa hatua ya awali. Na niwahakikishie kwamba nitaendelea kufanya teuzi kwa mtu ambaye ninaona ananifaa na si kwa kuangalia kabila, sura wala rangi."

"Kwa hiyo kama ninyi mna makundi mtajikuta mko mchanganyiko, mnakwenda kutumikia Watanzania na wanaochukia watanisamehe, uteuzi sio mwisho na bado tunaangalia utendaji wa walioteuliwa kama ni mzuri ataendelea kutumikia, lengo mimi kuteua Watanzania ambao nahisi tutasaidia kuhudumia wananchi."

Alisema mabadiliko ya mwaka huu alianza na timu ndogo, baadaye walikaa siku nzima kuangalia utendaji wa kila mmoja kuanzia wakuu wa mikoa, maRAC, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya (DAS) na wakurugenzi wa halmashauri.

Aliagiza kila ngazi watakaoteuliwa wafanyiwe mafunzo maalum, ili wanapokwenda kwenye utekelezaji wasiseme hawakujua kwenye utendaji.

"Niwashukuru waliotumikia nafasi yao na wakaondoka, wengine saba walioondoka ni kwa sababu mbalimbali, ila tutawatumia katika kazi nyingine, na wale wanajeshi walitakiwa kwenda kufanya kazi huko na ndiyo maana nikawatoa na kuteua wengine," alifafanua Rais Samia.

**MAELEKEZO**

Aliwaagiza viongozi hao kusimamia mapato na matumizi kwenye maeneo yao na kwamba hana msalie Mtume na kiongozi atayezembea katika hilo.

"Sina mswalie mtume kwenye mapato na matumizi, pesa nyingi tunazileta kwenye mikoa, wilaya kwa shughuli za maendeleo. Hapo nyuma niliwahi kusema watakao nijaribu katika hili wataniona rangi zangu, sasa nirudie tena kusema kwamba wataniona rangi zangu," alisisitiza.

"Kuna pesa nyingi zinashuka kwenye wilaya, zinaletwa kusukuma miradi ya maendeleo kwa wananchi, sio kucheza, kwa hiyo nataka zikafanye kazi hiyo."

Alikumbusha baadhi ya mikoa ambayo amewahi kutembelea kushuhudia kufanya vizuri na kutaka jambo hilo lifanyike katika mikoa mingine.

"Kwa mikoa ambayo nimewahi kutembelea, nimekuta kazi imefanyika japo kuna dosari kidogo, tunatoa pesa nyingi kwenye barabara, zile pesa zikatumike na kama kuna sababu ya kupeleka kwenye mradi mwingine, iandikwe," alisema.

"Kinachoonekana ni kwamba kuna mivutano kati ya wakuu wa wilaya, wabunge ma-DAS, wanapokaa na kujadili, kila mmoja anasema mradi upelekwe kule na mwingine anasema upelekwe kule, kwa hiyo mivutano haiishi mpaka inafikia hatua wanasema mradi upelekwe mwaka mwingine, hii sio sawa."

"Ukiuliza kuna nini, ni mvutano. Nataka mkaache mivutano kati ya DC, maDED, madiwani na wabunge, muache mivutano, fedha inapokuja kanuni zipo, sheria zipo ya kazi zinatakiwa kufanyika, mnavutana mradi uliokuwa ufanyike mwaka huu unasogezwa bila sababu za msingi."

Alitaka kupitiwa kwa viwango vya ukusanyaji mapato kwa kuwa walivyojipangia ni vidogo ambavyo vimeangalia mazoea ya nyuma na kwamba wote wakienda kwa nia moja itafanikiwa.

"Mwaka huu viwango tulivyojiwekea mmevuka kwa asilimia 103, mapato yakusanywe mkifanikiwa yale madogo tunayoyalilia yatafanikiwa."

Aidha, aliwataka viongozi hao kuhudumia wananchi kwa moyo safi na akili kwa kuwa hawana pa kuhudumia na kwamba wakifanya vizuri Mungu anawanyanyua na wakifanya ubaya ipo siku utajulikana.

"Katiba imeruhusu rais kutoa mamlaka kwa rais kugawa nchi vipande vipande na kutoa mamlaka kwa watu anaowaamini kuwakabidhi vipande vya nchi ili wavieendeshe. Mkuu wa mkoa ndiyo mkuu wa hilo eneo, walioko chini ni wako. Rais hana rafiki kwa hiyo na mwakilishi wake asiwe na rafiki, rafiki yake ni yule anayeitumikia nchi bali anayefanyakazi, anayetoa huduma kwa wananchi," alisema na kuongeza:

...Wananchi wanataka huduma zetu ndipo watakapojenga imani na nyinyi, sisi, kama umeaminiwa umekaa."

**KAZI IENDELEE**

Alisema wengi wanaitikia kazi iendelee, lakini hawajui viwango, kasi inayotakiwa na kusisitiza wataelekezwa kwenye mafunzo watakayopewa, ili waende kwenye njia sahihi.

**MABANGO YA CHALAMILA**

"Mwanangu Chalamila (Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert), mategemeo yangu umeukua sasa, akili imetulia, wewe ni mfanyakazi mzuri, lakini mtundu sana, nilikuacha nje kipindi hicho nimeamua kukurudisha, naomba ukakue akili itulie ukanisaidie huko ulikopangiwa, hii haina maana ndio umemaliza, kwamba ukikaa hapo umekaa, ukikaa hapo nakuangalia sana," alisema.

"Wale wanaokuja na mabango sasa kawaambie waandike tu, yapo maneno gani andikeni njooni nayo," alisema.

Alisema uzoefu unaonyesha wakisikia kiongozi anakwenda wanayakusanya mabango ya wananchi.

"Mnawanyima wananchi mdomo wa kusemea kama hutaki mabango nenda kafanye kazi yako, mwananchi akija na bango ndiyo mdomo wake wa kulalamika, mdomo wake mwingine ni mbunge, nilisema sitaki kuona mabango kwa maana mkafanye kazi zenu vizuri," alisisitiza.

**MASHIRIKA YA UMMA**

Alisema hayafanyi vizuri na kwamba huko nyuma walikuwa wanakopa ili kupeleka serikalini kuonekana wanafanyakazi na kwamba atafanya mabadiliko na kuweka mikakati kwa watakaofanikiwa kuaminiwa kuendelea na kazi.

Katibu Tawala wa Geita, Prof. Godius Kahyarara, alisema "Ninakwenda kusimamia rasilimali zilizoko kwenye Mkoa wa Geita, pamoja na kutekeleza maagizo niliyopewa na rais na waziri."

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya na Gwamaka Alipipi**

NYONGEZA YA MISHAHARA

## TUCTA yajiandaa kutoa tamko

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi nchini (TUCTA), lipo kwenye mchakato wa kuandaa vikao vya kikatiba kwa ajili ya kujadili majibu ya serikali ya nyongeza ya mshahara kwa watumishi wa umma ili kutoa tamko lake.

Hivi karibuni, serikali ilikuwa na majadiliano na TUCTA kutokana na malalamiko ya nyongeza hiyo ambayo kima cha chini kimeongezwa kwa asilimia 23.3.

Katika majadiliano hayo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitoa msimamo wa serikali kuhusu suala hilo na kudai kuwa nyongeza hiyo ililenga zaidi asilimia 75-78 ya watumishi wenye kipato cha chini.

Nipashe jana ilimtafuta Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, kuzungumzia majibu ya serikali na kusema: "Bado watumishi wanalalamika kuhusu hili na sisi hatuwezi kuja kujibu majibu ya hotuba ya Waziri Mkuu, kama sisi lazima tusubiri vikao vya kikatiba watakaposema basi sisi tutafikisha kwa wahusika."

"Tupo kwenye utaratibu wa kuviita vikao vya kikatiba na baada ya hapo ndiyo tutatoa tamko, kwa sasa siwezi kujibu peke yangu, natakiwa nitoe majibu ya wenye chama," alisisitiza.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika kikao kilichokutanisha serikali na viongozi wa wafanyakazi, Waziri Mkuu Majaliwa, alisema kwenye upandishaji wa mishahara kuna utaratibu unaotumika, wanapopandisha mishahara kima cha chini maana yake wanaangaliwa wafanyakazi wa kipato cha chini.

"Tukisema kima cha chini kinasaidia kupeleka mwelekeo hata kwenye sekta binafsi kwamba na huko mishahara kima cha chini kianzie hapo sasa ile asilimia inayotamkwa inawalenga zaidi wale wenye kima cha chini sio tu wale wanaoanza kazi hata waliotangulia kazi ambao wapo kwenye kima cha chini kwa lengo la kuinua kiwango chao ili wapate fedha ambayo inaweza kukidhi mahitaji yao kutokana na mabadiliko ya uchumi nchini."

"Huku juu kwa watumishi wenye mapato makubwa hawapati ile asilimia kama inavyotamkwa tukiwalipa ile watakuwa wamekwenda mbali zaidi kuliko hawa wenye kipato cha chini kwa hiyo gap (pengo) la mishahara ndani ya serikali litakuwa kubwa," alisema.

Majaliwa alisema inatakiwa asilimia ipungue ili kuweka usawa wa mishahara na kuwaweka kwenye mfumo ambao hauweki pengo kubwa.

Hata hivyo, alisema upandishaji huo unafanyika kwa kuangalia hali ya uchumi nchini ili kutokwamisha kufanyika mambo mengine.

"Hawa wanaosema tumeongezwa Sh. 20,000 ni wenye mishahara mikubwa wapo kwenye hii asilimia 22, humo ndiyo unawakuta Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi, Mameneja mashirika ambao na wao kidogo wana mshahara unaotosha."

"Ni asilimia 22 tu, katika hili viongozi wenzangu wa wafanyakazi hawa ndiyo wamemudu hili jambo mpaka inaonekana ni tatizo, lakini waliolengwa hii asilimia 23 hadi kushuka 20 ni asilimia 75," alisema.

Julai 26, mwaka huu, Serikali na TUCTA walikutana kwa ajili ya kujadili suala la mshahara uliolipwa mwezi Julai mwaka huu ambalo wafanyakazi walionesha kutoridhishwa.

Miongoni mwa hoja zilizowasilishwa na TUCTA kwa serikali ni kiwango cha kima cha juu cha mshahara kisipungue asilimia 15.

Aidha, baadhi ya kada na taasisi za umma ambazo hazijaguswa na nyongeza hiyo ziangaliwe.

**HABARI KITAIFA**

# Jamhuri yaomba kibali kesi meno ya tembo isikilizwe mfululizo

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kukutwa na vipande 660 vya meno ya tembo vyenye thamani ya Sh. bilioni 4.5 inayowakabili washtakiwa 11, umeomba kibali Mahakama Kuu ili kesi hiyo ipangiwe kikao cha kusikilizwa mfululizo.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Wakili wa Serikali, Esther Martin, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ngimilanga wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa.

Martin alidai kuwa wamefikia hatua hiyo kutokana na changamoto iliyojitokeza kwa upande wa mawakili wa utetezi kushindwa kufika mahakamani kuendelea na kesi hiyo kwa sababu wanakwenda kwenye kesi zingine Mahakama Kuu.

Alidai kisheria inaruhusu, hivyo wanatakiwa waende mahakama za juu kutokana na hali hiyo kesi hiyo imekuwa ikiahirishwa mara kwa mara kwa sababu inahusisha mawakili wengi.

"Tumeambiwa bado kuna changamoto ya mawakili wa utetezi, ndiyo maana hatuna shahidi kwa leo (jana), kwa hiyo tunaomba kesi ipangiwe Agosti 16, mwaka huu ili tuone kama maombi yetu ya Mahakama Kuu yamekubaliwa," alidai Martin.

Hata hivyo, mmoja wa mawakili wa utetezi, Twaha Tasilima, alidai wapo tayari kuendelea na mpango wa upande



wa mashtaka.

Hakimu Ngimilanga alikubali ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Agosti 16, mwaka huu kwa kutajwa.

Kesi hiyo ya uhujumu uchumi inamkabili mfanyabiashara Ally Anguzuu raia wa Guinea, mfanyabiashara Victor Mawala, Haruni Abdallah, Abbas Hassan na Solomoni Mtenya.

Washtakiwa wengine ni Khalfani Kahengele, Ismail Kassa, Juma Buguma, Kassim Said, Peter Nyachiwa, John Buhanza na Mussa Abdallah wote wakazi wa Dar es Salaam.

Katika kesi hiyo, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka ya kujihusisha na nyara za serikali bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori, ambazo ni meno hayo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 4.6.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa na mtandao mkubwa wa uhalifu wa ujangili ambao unajihusisha kuuza, kununua, kupokea, kuhamisha, kusafirisha nyara za serikali ambazo ni meno ya tembo.

# Kiwanda cha parachichi chatoa ajira zaidi 200

**Na Mwandishi Wetu**, RUNGWE

SERIKALI imesema kuwa wananchi wilayani Rungwe, wameanza kunufaika na uwekezaji wa viwanda baada ya umeme kufika vijijini na sasa kuna kiwanda cha parachichi kimeajiri watu 230.

Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema hayo alipotembelea kiwanda cha kusindika mafuta yatokanayo na parachichi cha Kuza Africa Limited, ambacho kinanunua malighafi ya zao hilo kwa wakulima ambao wanashindwa kuuza nje ya nchi.

"Maparachichi yanalimwa kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi. Kabla ya kusafirishwa yanakaguliwa, nusu ambayo mkulima angepoteza, yananunuliwa na kuletwa hapa. Kwa hiyo kama mkulima amelima tani 20 alikuwa anapata pesa ya tani 10 sasa anapata pesa ya tani zote 20 kwa sababu kuna mahali yanachukuliwa," alifafanua.

Alimpongeza mwekezaji wa kiwanda hicho kwa kutumia fursa ya umeme kuzalisha ajira zaidi ya 30 kiwandani na 200 shambani na kwamba hilo limewezekana kutokana na uwapo wa umeme wa uhakika.

Kwa upande wake mwekezaji wa kiwanda hicho, Rob Clowel, aliishukuru serikali kwa kumuunganishia umeme ambao umerahisisha uzalishaji.

Naye Mkuu wa Wilaya Rungwe, Dk. Vicent Mwantona, alisema awali kulikuwa na changamoto ya transfoma, lakini ilitatuliwa na TANESCO kuhakikisha umeme wa kutosha unapatikana.

"Huyu ni mwekezaji na ameajiri watu wa ndani na wengine wanaletwa kutoka kwenye mashamba yao, kwa hiyo ni lazima asaidiwe," alisema.

Alisema kutokana na wilaya hiyo kuzalisha maparachichi kwa wingi, kipaumbele ni kuongeza thamani ili kurahisisha upatikanaji wa masoko.

"Kwa mfano mwaka huu bei ya parachichi iliyumba, unapeleka wapi? Lakini ukienda kwenye mnyororo wa mafuta unawasaidia wakulima," alisema.

Dk. Anney alisema kufikishwa kwa umeme kumewezesha kujengwa kwa viwanda vingi wilayani humo.

Awali, Meneja wa TANESCO, Wilaya ya Rungwe, Mhandisi Muhsin Kijemkuu, alisema mwekezaji huyo alikuwa akitumia umeme wa njia tatu, ambayo ilikuwa inashindwa kuendesha mitambo yake.

"Kabla ya kumfungia transfoma yake alikuwa akizalisha mafuta lita 2,000 kwa siku, lakini baada ya kumfungia mpango wake ni kuzalisha lita 4,000 kwa siku. Alikuwa akitumia Sh. 700,000 kwa siku kwa ajili ya gharama za nishati ya umeme sasa anatumia Sh. 100,000 tu kwa siku sawa na Shilingi milioni tatu kwa mwezi," alifafanua.

"Kwa siku alikuwa anatumia lita 250 za dizeli sawa na lita 7,500 kwa mwezi na alikuwa analipa Sh. milioni 24 kwa ajili ya mafuta, lakini baada ya kumfungia umeme gharama zitashuka," aliongeza.






Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akitoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Geofrey Mkamilo, kuhusu kutumia utafiti ili kuinua mazao mbalimbali nchini ikiwamo zao la parachichi katika mikoa mbalimbali ikiwamo Dodoma wakati akitembelea banda la Wizara ya Kilimo katika Maonyesho ya Nanenane 2022 yanayofanyika katika Uwanja wa John Mwakangale mkoani Mbeya jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Matumizi tiketi kielektroniki mabasi mkoani yasuasua

**Na Jenifer Gilla**

AGIZO la Mamlaka ya Udhibiti na Usafiri Ardhini (LATRA) la kutaka mabasi yote yanayoenda mikoani kuanza kutumia tiketi za kielektroniki, halijaanza kutekelezwa kwa baadhi ya mabasi huku mashine zinazotolea tiketi hizo zikiwekwa pembeni.

Mwandishi wa gazeti hili jana alipiga kambi katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Mbezi jijini Dar es Salaam na kushuhudia baadhi ya ofisi zikiendelea kutoa tiketi za kawaida, huku wengine wakisingizia uchache wa mashine na kuwaahidi abiria kuwapa tiketi za kielektroniki ndani ya mabasi.

Katika ofisi za magari yaendayo mikoa ya Kaskazini, Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini, Nipashe pia ilibaini tiketi za kawaida kuendelea kutumika.

Hali hiyo imejitokeza huku juzi ikiwa siku ya mwisho kwa magari kutumia tiketi za kawaida na LATRA ikitangaza kufanya tathmini na kuchukua hatua kali kwa wasiotekeleza.

Julai 26, mwaka huu, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, kupitia taarifa yake kwa umma alisema kikao cha tathmini walichofanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), waliazimia hadi juzi mabasi yote yatumie mfumo wa kutoa tiketi kielektroniki.

Aidha, alisema jumla ya mabasi 550 yameunganishwa kwenye mfumo huo na kwamba kwa siku yanakatisha wastani wa tiketi 5,000 hadi 7,000.

Katika moja ya ofisi ya mabasi yaendayo Kigoma, Nipashe ilishuhudia mashine ya kielektroniki ikiwa mezani, huku msafiri akikatiwa tiketi kawaida.

"Mashine bado haijaanza kutumika dada, mpaka wiki ijayo, kuna marekebisho zinatakiwa zifanyiwe zitaanza kutumika wiki ijayo. Kwani ukichukua hii ya karatasi kuna shida gani? Zote si tiketi na zinatambulika," alihoji mhudumu huyo, mwandishi aliposisitiza kukatiwa tiketi ya kielektroniki.

Katika ofisi ya mabasi yaendayo mkoani Shinyanga, mwandishi alitaka kukatiwa tiketi ya kusafiri siku inayofuata na kuambiwa atapewa ya kawaida hadi siku ya safari akishapanda kwenye basi atapewa ya kielektroniki.

"Ungekuwa kama ni msafiri wa leo tungekupa tiketi, lakini kwa kuwa unataka kusafiri kesho tunakupa tiketi ya kawaida halafu kesho ukiwa ndani ya gari tutakupa ya kielektroniki," alisema mhudumu huyo ambaye hakutaka kutaja jina lake.

Katika ofisi za mabasi yaendayo Mwanza, mwandishi alijibiwa: "Mashine ina hitilafu ya kimtandao dada, lakini hakuna tatizo lolote, tutakupatia tiketi hii ya zamani ili uwe na uhakika wa safari halafu kesho ukija tutakupa ya kielektroniki."

Mmoja wa wakala wa mabasi yanayokwenda Tanga, Maiko James, alisema kinachosababisha baadhi ya mawakala kutotumia mashine hizo ni kukosekana za kutosha na baadhi kununua chache wanazotumia kwa wateja wa gari linalosafiri siku hiyo pekee.

"Kwa mantiki hiyo inabidi hizo mashine watembee nazo kwenye magari kwa sababu trafiki wanakagua. Wanaopata ni hao wa kwenye magari hawa wanaokata kwa siku zijazo inabidi wawape tiketi za kawaida halafu wakiwa kwenye magari wanapewa za kielektroniki," alisema.

Wakala wa mabasi yaendayo Korogwe, Shabani Hamdani, alisema sababu nyingine ni kuwa mashine hizo zinatumia muda mrefu kuhudumia wateja tofauti na tiketi za karatasi hali inayopoteza muda hata wa magari kuondoka.

"Mashine zina changamoto ya kukusubirisha dada yangu, tofauti na ukiandika kwa mkono, wateja wengi ni wale wa kuondoka siku hiyo hiyo wanakuja hapa wanajazana kwenye ofisi mashine zinachelewesha sana, kuna siku mtandao unagoma nazo hazifanyi kazi," alisema.

Mmoja wa abiria, Athat John, aliyekata tiketi ya kwenda Korogwe, alikiri kupewa tiketi ya zamani na alipoulizwa kutokuwa na tiketi ya kielektroniki alisema:

"Sina taarifa kama kuna tiketi mpya kwa sababu sijasafiri muda mrefu. Mimi niwewapa hela wakanipa tiketi hii nikaondoka nitakuja kesho kupanda gari, wakinikana ndio tutajuana hapo hapo."

**TABOA WAZUNGUMZA**

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Mustapher Mwalongo, alisema kuwa mwitikio wa mawakala kuhusu mfumo huo ni mkubwa na changamoto zote zimetatuliwa.

"Mwitikio wa mawakala ni mzuri, sisi tunaendelea kuhamasisha mawakala. Changamoto zote zilizokuwa zinatuzuia kusonga mbele tumeshazifanyia kazi. Ma-vendor (watoa mashine) wapo wa kutosha mikoani kwa ajili ya kuwahudumia mawakala wa huko," alisema.

**MSIMAMO WA SERIKALI**

Ofisa Biashara wa Kituo cha Mabasi ya mkoani, Geofrey Mbwana, alisema wanaendelea kuhamasisha matumizi ya tiketi za kielektroniki kwa wasafiri na wadau wengine.

"Nafikiri hata wewe umesikia hayo matangazo, tunawaelimisha abiria kuwa ni lazima wawe na tiketi za mfumo wa kielektroniki na atakayekuwa na tiketi tofauti tunamhesabu kama msindikizaji na atalazimika kulipia mlangoni," alisema.

Aidha, Suluo alisema kuwa matumizi ya tiketi za kielektroniki yamelenga kuwanufaisha wasafirishaji kwa kuwa watadhibiti mauzo ya tiketi na mfumo unawawezesha kuona mauzo yote yanayofanyika kupitia simu za mkononi.

Alisema serikali itanufaika kwa taarifa zinazozalishwa na mfumo kwa kupata taarifa mbalimbali zitakazosaidia kufanya uamuzi muhimu ukiwamo wa kuboresha huduma, miundombinu na kukokotoa kodi ya mapato.

## Serikali yapiga 'stop' vipimo lumbesa

**Grace Mwakalinga na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amepiga marufuku ununuzi wa mazao ya wakulima kwa kutumia vipimo visivyokuwa rasmi ikiwamo ujazo uliozidi (lumbesa).

Alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizindua Maonesho ya Wakulima (Nanenane) ambayo kitaifa yanafanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini hapo.

Dk. Mpango alisema, kuanzia sasa mazao yote yanatakiwa kuuzwa kwa kupimwa kwenye mizani huku akiwataka wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya zote nchini kusimamia matumizi ya vipimo hivyo.

Alisema hata mifugo inatakiwa kuuzwa kwa kutumia mizani na kuagiza ielekezwe kwenye minada yote ya mazao ili itumike kupima mazao ya wakulima.

"Kuanzia sasa lumbesa nchini 'no' (hapana), kwa hiyo mazao yote yatanunuliwa kwa kutumia mizani, nawaagiza wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya msimamie hili, hatutaki kusikia mahali popote biashara hii ikiendelea," alisema Dk. Mpango.

Alisema faini za lumbesa hazitatakiwa kuwa chanzo cha kuendelea kutumika kwa vipimo hivyo visivyostahili kwenye ununuzi wa mazao ya wakulima.

Katika hatua nyingine Dk. Mpango aliiagiza Wizara ya Kilimo kufanya tathmini ya hali ya chakula nchini ili kuepuka kutokea kwa tatizo la upungufu wa chakula nchini.

Vilevile, aliwataka Watanzania kutunza akiba ya chakula badala ya kuuza kila kitu na kuanza kuhangaika baadaye kununua kwa bei ya juu.

Aliziagiza Taasisi za Utafiti wa Kilimo ikiwamo, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) kufanya utafiti wa mazao yanayostawi kwenye maeneo mbalimbali nchini ili kuondokana na kilimo cha mazoea kinachoainisha kuwa baadhi ya mazao yanastawi kwenye baadhi ya mikoa na mingine hayastawi.

Pia Dk. Mpango alisema serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuimarisha sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo kama mbolea, mbegu na dawa za kuua wadudu.

Alisema serikali imerejesha utaratibu wa ununuzi wa pamoja wa mbolea ili inunuliwe kwa wingi na kushusha bei ambayo wakulima wote watakuwa na uwezo wa kununua.

Dk. Mpango aliiagiza Taasisi ya Teknolojia nchini (DIT) pamoja na Shirika la Kusimamia Viwanda Vidogo (SIDO) kubuni teknolojia zitakazosaidia kuhifadhi mazao yanayoharibika shambani.

Alisema kumekuwa na tatizo la mazao ya wakulima kuharibika yakiwa shambani na baada ya kuvunwa kabla ya kuuzwa hali inayosababisha wakulima kupata hasara hivyo uwapo wa teknolojia hiyo itasaidia wakulima kutunza na kuhifadhi mazao yao wakati wakisubiri soko la uhakika.

Awali Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alimwomba Makamu wa Rais, kutoa tamko la kuzuia matumizi ya vipimo visivyo rasmi kwenye ununuzi wa mazao ikiwamo ujazo unaozidi ambavyo vinawaumiza wakulima.

"Wizara ya Kilimo tumelizungumza sana suala la lumbesa lakini hadi sasa linaendelea na baadhi ya halmashauri zimeweka ni kitega uchumi, zinawakamata wafanyabiashara na kuwatoza faini wakati wakulima wanakuwa tayari wameumia," alisema Bashe.

"Wakati mwingine yawezekana utekelezaji unakuwa mdogo kwa sababu maagizo tunatoa sisi, labda mtusaidie nyie viongozi wetu wakubwa kutoa tamko," aliongeza.

Aidha, Bashe alisema kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wafanyabiashara wanapozuiliwa kununua mazao kwenye eneo moja kwa kutumia vipimo hivyo, wanakimbilia maeneo mengine na kusababisha mazao ya wakulima kwenye eneo husika kukosa soko.

Katika hatua nyingine Waziri Bashe alisema wizara yake imeunda kamati maalumu ya kufuatilia mifumo ya utoaji wa mikopo kwa wakulima kwenye benki mbalimbali ili kuifanyia marekebisho mifumo hiyo.

## TANGAZO

# PUBLIC NOTICE

**Following the amendment of Section 46A of the National Payment Systems Act, Cap. 437 by the Finance Act,2022 and the coming into force of National Payment Systems (Electronic Money Transaction Levy) Regulations, 2022 prescribing the manner and modality under which the electronic money levy is to be collected, we hereby inform our esteemed subscribers of applicable Tigo Pesa Tariffs that comprise of government levy effective 1st July, 2022**

*In this effect please see the below new tariffs from Tigo Pesa that includes the new government levy*

## tigo pesa — Ni Zaidi ya Pesa

## Ada za wateja. Piga *150*01#

| Kiwango (Tsh) | | Kutuma pesa kwenda Tigo Pesa | | | Kutuma pesa kwenda mitandao washirika | | | Kutoa pesa kwa Wakala/ATM | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzia | Mwisho | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato |
| 100 | 999 | 15 | 10 | 25 | 5 | 10 | 25 | - | 10 | 10 |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 10 | 40 | 45 | 10 | 55 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 30 | 10 | 40 | 45 | 10 | 55 | 400 | 10 | 410 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 15 | 65 | 90 | 15 | 105 | 600 | 15 | 615 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 30 | 90 | 90 | 30 | 120 | 650 | 30 | 680 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 60 | 190 | 180 | 60 | 240 | 950 | 60 | 1,010 |
| 7,000 | 9,999 | 150 | 70 | 220 | 180 | 70 | 250 | 1,000 | 70 | 1,070 |
| 10,000 | 14,999 | 360 | 128 | 488 | 495 | 128 | 623 | 1,450 | 128 | 1,578 |
| 15,000 | 19,999 | 360 | 243 | 603 | 495 | 243 | 738 | 1,450 | 243 | 1,693 |
| 20,000 | 29,999 | 380 | 383 | 763 | 540 | 383 | 923 | 1,850 | 383 | 2,233 |
| 30,000 | 39,999 | 400 | 439 | 839 | 612 | 439 | 1,051 | 1,850 | 439 | 2,289 |
| 40,000 | 49,999 | 410 | 599 | 1,009 | 675 | 599 | 1,274 | 2,350 | 599 | 2,949 |
| 50,000 | 99,999 | 720 | 818 | 1,538 | 1,125 | 818 | 1,943 | 2,700 | 818 | 3,518 |
| 100,000 | 199,999 | 1,000 | 1,009 | 2,009 | 1,440 | 1,009 | 2,449 | 3,650 | 1,009 | 4,659 |
| 200,000 | 299,999 | 1,200 | 1,173 | 2,373 | 1,710 | 1,173 | 2,883 | 5,300 | 1,173 | 6,473 |
| 300,000 | 399,999 | 1,500 | 1,397 | 2,897 | 2,070 | 1,397 | 3,467 | 6,500 | 1,397 | 7,897 |
| 400,000 | 499,999 | 1,500 | 1,636 | 3,136 | 2,250 | 1,636 | 3,886 | 7,000 | 1,636 | 8,636 |
| 500,000 | 599,999 | 2,200 | 2,075 | 4,275 | 2,880 | 2,075 | 4,955 | 7,500 | 2,075 | 9,575 |
| 600,000 | 699,999 | 3,300 | 2,554 | 5,854 | 3,870 | 2,554 | 6,424 | 8,000 | 2,554 | 10,554 |
| 700,000 | 799,999 | 3,300 | 2,833 | 6,133 | 3,870 | 2,833 | 6,703 | 8,000 | 2,833 | 10,833 |
| 800,000 | 899,999 | 3,500 | 3,000 | 6,500 | 3,870 | 3,000 | 6,870 | 8,000 | 3,000 | 11,000 |
| 900,000 | 1,000,000 | 3,500 | 3,551 | 7,051 | 5,400 | 3,551 | 8,951 | 8,000 | 3,551 | 11,551 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 5,000 | 3,751 | 8,751 | 5,400 | 3,751 | 9,151 | 8,000 | 3,751 | 11,751 |
| 3,000,001 | 10,000,000 | 5,000 | 4,000 | 9,000 | 5,400 | 4,000 | 9,400 | 10,000 | 4,000 | 14,000 |

| Tukio | Kuanzia | Mwisho | Ada |
|---|---|---|---|
| Kuweka pesa | 1,000 | 5,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | Ada ya kutuma + Ada ya kutoa |
| Kutoa Pesa kwa mteja ambaye amesajiliwa ila hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwenda nchi za nje | 100 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |
| Malipo kwa Tigo Pesa | 500 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |

| Tukio | Ada |
|---|---|
| Kubadilisha namba ya siri | BURE |
| Kuangalia salio/ Taarifa ndogo | 50 |
| Kurudisha muamala uliokosea (Jihudumie) | 50 |
| **Kupata taarifa ya mwezi** | **Ada** |
| Taarifa ya Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |
| Taarifa ya Miezi 3 | 1,000 |
| Taarifa ya Mwaka 1 | 2,000 |

Kwa vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-standard-terms-and-conditions. **Ada zote zimejumuisha kodi zote zinazohusika.**
Kwa Ada za huduma nyingine tembelea tovuti; **https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-tariffs**

**Furahia Malipo kwa Tigo Pesa:** LIPA KWA SIMU

**KUMBUKA:**
1. Unaweza kuweka au kupokea hadi TSh 10,000,000 kwa siku na unaweza kutoa au kutuma hadi TSh 5,000,000 kwa siku, pia unaweza kuhifadhi hadi TSh 10,000,000 kwa wakati mmoja kwenye akaunti yako ya Tigo Pesa, kama usajili wako umekamilika.
2. Onesha kitambulisho chako kabla ya kuweka au kutoa pesa kwa Wakala.
3. Hakikisha taarifa zako za usajili ni sahihi kwa kupiga *106# kisha 2 au piga huduma kwa wateja kwa maelezo zaidi.
4. Hesabu pesa zako na hakikisha salio lako la Tigo Pesa linaendana na muamala uliofanya kabla ya kuondoka kwa Wakala.
5. Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
6. Hakikisha unahifadhi namba yako ya siri (PIN), simu yako na laini yako kwa usalama. Usimpe (PIN, Simu, laini yako) wala kumtajia mtu yoyote namba yako ya siri, iwe Wakala wa Tigo Pesa, mfanyakazi wa Tigo au mhudumu wa Tigo Huduma kwa wateja. Pia kumbuka kubadili namba yako ya siri mara kwa mara.
7. Tigo itakupigia kwa 100 Tu.
8. Kutoa taarifa yoyote dhidi ya udanganyifu Piga simu namba 100 au tuma ujumbe kwenda namba 15040 au kwa barua pepe kwenda customercare@tigo.co.tz
9. Unaweza kupokea pesa kutoka nchi zaidi ya 200 duniani, na unaweza kutuma pesa kwenda nchi zote za Mashariki na Kusini mwa Afrika.
10. Kupata vigezo na masharti ya kutumia Tigo Pesa, tembelea duka la Tigo lililopo karibu nawe au www.tigo.co.tz

Unaweza kurudisha **muamala uliokosea, token ya luku, ku-unbar akaunti yako ya Tigo Pesa** na **kuriseti PIN**

Piga ***150*01#** chagua **6 (Jihudumie)** kisha chagua huduma unayotaka

tigo pesa

**App yenye urahisi wa kushangaza!**




**Fanya malipo ya Serikali**

DAWASA LUKU

Pakua kwenye

Google Play | App Store

tigo pesa

Kuwasaliana na huduma kwa wateja,
Piga **100** bure au tembelea duka lolote la Tigo!
Ada hizi ni kuanzia Julai 2022

tigo

www.tigo.co.tz

216973501

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili la polisi Mbeya ni darasa bora, tuige

**KATIBA** ya Tanzania ya 1977 na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, vinamlinda kila mtoto dhidi ya unyanyasaji wa aina yoyote kama kutelekezwa, kudhuriwa, mila kandamizi, desturi zenye madhara na kazi hatarishi au za unyonyaji.

Aidha, Tanzania imeridhia mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto na Mikataba ya Shirika la Kazi (ILO) kuhusu ulinzi na hifadhi za watoto wenye umri wa chini wa kuajiriwa kwa ajira zinazoruhusiwa na mbaya zinazokatazwa.

Tunatoa angalizo hili, tukirejea maagizo ya Polisi Mkoa wa Mbeya kuwasaka na kuwafikisha mbele ya sheria wazazi na walezi watakaowatumia watoto wao kinyume cha sheria kwenye maonyesho ya Nanenane mkoani humo.

Ni taarifa iliyochapishwa na gazeti hili jana.

Tunaungana na polisi kwenye hilo, licha ya kuwapo sheria hizo, watoto wanakabiliwa na aina mbaya zaidi za ajira ikiwamo kutumikishwa nyumbani (house girls na boys) kwenye kila aina ya unyanyasaji na ukatili mkubwa.

Tunasikia kilio cha wanaotumikishwa kingono na hata kuuzwa ughaibuni, wakati mwingine hutokana na biashara haramu ya binadamu wanakwenda kufanyakazi kwenye madanguro. Watoto pia wanatumiwa kwenye ajira katika kilimo, wanalima mashambani kwa ujira kiduchu au bila malipo, aidha hufanya shughuli za kumwagilia mazao kwa kushika sumu na vihatarishi vya ajili ya kuua wadudu na zote ni shughuli ngumu zinazotishia ustawi wao.

Watoto wanafanyishwa kazi za kulazimishwa na hutumia vihatarishi haswa katika shughuli za migodini kutumia kemikali mfano zebaki kuchenjulia dhahabu.

Aidha, katika zama hizi watoto wengi hudhulumiwa kingono kutokana na biashara haramu ya binadamu inayofanyika ndani na nje ya nchi, hivyo husababisha wavulana na wasichana kuathirika kisaikolojia kwa kutumikishwa katika biashara za kingono hususan maeneo yenye mzunguko mkubwa wa biashara.

Watoto si kwamba wananyanyaswa nje ya familia zao pekee, hata ndani ya nyumba kuna baadhi ya wazazi na walezi wanawatumia kuuza bidhaa mbalimbali ili kuleta kipato kwa familia. Mara nyingi wazazi wanaambiwa kuwa kuwatumikisha watoto maeneo kama hayo husababisha kunajisiwa na kufanyiwa unyanyasaji wa kingono.

Jeshi la Polisi mkoani Mbeya limekumbusha wajibu wa wazazi katika malezi ya watoto kutowahusisha kwenye uuzaji wa bidhaa katika maonyesho ya Nanenane, hivyo nasi si budi kuukumbusha umma kuwa ni vibaya watoto kutumiwa kwenye sherehe au maonyesho na shughuli zote zinazozidi umri wao.

Tunakumbusha kuwa si vyema kuwatumia katika shughuli mbalimbali za kijamii kwenye matangazo ya biashara kuanzia runinga, mabango mitaani na hata tamthilia. Tunaona kuwa wanaofanya hivyo wananufaika zaidi kuliko watoto kwa vile ni wadogo na hawaelewi kitu wala hawawezi kuingia mikataba.

Tunaona kuwa kwenye muziki watoto wanatumiwa kucheza wakigeuzwa kuwa wahusika kwenye nyimbo au tungo, lakini pia tunawaona wakitumiwa kutoa buruduni kwenye sherehe ambazo hualikwa kuimba au kucheza na kutunzwa fedha kwa kisingizio kuwa ni wahitaji wanahitaji msaada.

Hata hivyo haifahamiki iwapo fedha hizo wanazochangiwa watazipata zote au watagawana na aliyewaleta au mshereheshaji (MC). Tunasisitiza kuwa ni muhimu na lazima kuwalinda watoto kama katiba, sheria na ILO zinavyoelekeza.

Kwa kuwa hawa ndiyo Watanzania wa kesho, hivyo tuwajibike maana taifa lisilolinda watoto wake ni sawa na taifa lililojimaliza na lisilojijali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Christina Haule

## Muungwana Lazima Nilonge

# Viongozi wakisimamia sheria wataokoa misitu

**VIONGOZI** wa serikali kuanzia ngazi za mitaa, vijiji, wilaya, mkoa hadi taifa wakati umefika kuhamasisha na kusimamia jamii kufuata sheria za misitu zilizoko wanapoandaa mashamba ili kuepuka ukataji miti ovyo unaosababisha upotevu wa misitu, ukame na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi.

Mhifadhi mwandamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) Manispaa na Wilaya ya Morogoro, Faustine Msokwa anasema kuwa jamii imekuwa haiangalii mambo ya maendeleo ya baadaye kwa ajili yao na taifa bali hukata miti kwa juhudi zote lakini bila kupanda mingine.

Miti inayokatwa ni kwa ajili ya kusafisha mashamba na kuanza kilimo jambo ambalo lina manufaa kifedha kwa muda mfupi, lakini likichangia ukame na athari nyingine zitakazolikumba taifa kwa muda mrefu.

Suala la ukataji miti ovyo na uchomaji mkaa linasababishwa na viongozi wa vijiji ambao ndio wana umiliki wa ardhi za vijiji kutokuwa na makini tena bila kuweka msisitizo ikiwamo sheria ndogo na taratibu za matumizi ya ardhi hiyo ili kuendelea kubaki kuwa endelevu, anaonya Msokwa.

Taasisi kama TFS zinasisitiza usimamizi shirikishi wa mazao ya misitu (USMJ) unaotaka ushiriki wa wadau wote wa misitu ambao ni pamoja na wakulima na wafugaji ambao wamekuwa wakivamia maeneo na kudai wanasafisha kwa kilimo au kukaa na mifugo huku wakikata miti ambayo inatakiwa kuhifadhiwa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Anasema licha ya kukamatwa wahalifu hao wa misitu wanaofikia hata 50 kwenye mashamba wanaodai wanaandaa mashamba kwa kuwa wana kibali cha kijiji, lakini ukifuatilia miti wanayoikata wanachoma mkaa pia hawapo wenye vibali vya kusafisha shamba au hata kama wapo ni wachache, jambo ambalo ni hatari kwa uhifadhi wa misitu.

**Hamasa ya ufugaji nyuki katika wilaya ya Morogoro imekuwa ndogo kutokana na ukosefu wa elimu na kwamba TFS ipo tayari kumsaidia mtu mmoja mmoja au kikundi kielimu na mizinga bure iwapo atajitokeza ili aweze kufuga nyuki na kuhifadhi mazingira.**

Yote hayo inaonyesha udhaifu wa viongozi vijijini katika kusimamia rasilimali mfano misitu, maji na ardhi mambo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya wanavijiji na taifa pia.

Ni ukweli kwamba ukataji miti ovyo na uchomaji wa mkaa bila kufuata utaratibu unazifanya hata manispaa na wilaya kushindwa kukadiria kiwango cha mkaa kinachohitajika kutumika kwa jamii hizo.

Hata hivyo upo mkanganyiko unaorudisha nyuma suala la usimamizi shirikishi wa mazao ya misitu (USMJ) ikiwamo sera mtambuka za Wizara ya Maliasili na Utalii zinazohamasisha uhifadhi wa misitu wakati kilimo kinahamasishwa wakulima kupanua mashamba kwa ajili ya kilimo endelevu.

Aidha, ni vyema wanajamii wakahamasishwa kujitokeza kupata elimu ya ufugaji nyuki na kupata mizinga bure kwa sababu ufugaji wa nyuki una tija zaidi tena kubwa tofauti na ufugaji unaoweza kukaa na wanyama kwa miongo kadhaa lakini bila faida ya muda mfupi, lakini kwa kuvuna asali kila baada ya miezi mitatu au sita kwa mwaka na kupata masoko ya ndani na nje ya nchi wakati wanyama hawana mavuno hayo.

Ofisa wa TFS mhifadhi mwandamizi wa Manispaa na Wilaya ya Morogoro, Faustine Msokwa, anasema hamasa ya ufugaji nyuki katika wilaya ya Morogoro imekuwa ndogo kutokana na ukosefu wa elimu na kwamba TFS ipo tayari kumsaidia mtu mmoja mmoja au kikundi kielimu na mizinga bure iwapo atajitokeza ili aweze kufuga nyuki na kuhifadhi mazingira.

Hilo ni suala ambalo linapaswa kusambazwa kwa mikoa na maeneo mengi watu wanapong'ang'ania ufugaji kuachana na kufuga wanyama kwa wingi na badala yake wajikite kwenye kuzalisha asali ambayo ina faida na ni rafiki wa mazingira na pia ni muhimu kwa afya ya binadamu na pia ni tiba.

# Mganga adaiwa kumwogesha dawa ya mapenzi mwanafunzi kisha kumtorosha

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

MWANAFUNZI wa kidato cha pili Shule ya Sekondari Usule, Kata ya Usule, Halmashauri ya Shinyanga mwenye umri wa miaka 17 (jina limehifadhiwa), anadaiwa kutoroshwa na mganga wa jadi aliyetokea Tanga na kwenda naye kusikojulikana.

Imedaiwa kuwa mganga huyo alifika kwenye kata hiyo kuwaogesha dawa za mvuto wa mapenzi maarufu 'samba' wanafunzi na mabinti walio katika umri wa balehe ili wapate wanaume wa kuwaoa kwa kuwashirikisha wazazi wao.

Mratibu wa mradi wa Tuwawezeshe kutoka Shirika lisilo la kiserikali la Rafiki-Sdo, mkoani Shinyanga, Maria Maduhu, aliyabainisha hayo jana wakati akitoa taarifa ya tathmini ya ufungaji wa mradi wa kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, uliofadhiliwa na Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Alisema wakati wa utekelezaji wa mradi huo, walikutana na visa viwili vikubwa vilivyowashirikisha wazazi, kikiwamo cha watoto kuogeshwa dawa na mganga na kutoroka na mwanafunzi huyo.

Aidha, alidai kuwa kisa cha pili ni cha mwanafunzi wa Kata ya Ilole, aliyeogeshwa dawa hizo na kupata mwanaume wa kumuoa na baada ya siku kadhaa ndoa ilivunjika na mwanafunzi huyo kubainika kuwa na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Alisema walifanikiwa kuwafikia zaidi ya wananchi 263 katika kata za Ilole na Usule na kuwapatia elimu ya mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Mkurugenzi wa Shirika la AGAPE, John Myola, alidai kuwa waganga wa jadi wanawahadaa wazazi kuwa baada ya mtoto kuogeshwa dawa za mvuto wa mapenzi mwanaume yeyote atayekutana naye barabarani na kumsemesha atakuwa mume wake. Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Deus Mhoja, alisema matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na wanawake bado yapo juu katika halmashauri hiyo na kwamba wataendelea kupambana ili kuhakikisha yanakwisha kabisa.

Alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023, halmashauri hiyo imetenga Sh. milioni 21 kwa ajili ya kuendeleza mabaraza ya watoto, majukwaa ya wanawake katika kata zote.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Mfuko wa Wanawake mkoani Shinyanga, Glory Mbia, aliiomba serikali kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali kuendelea kupambana na ukatili wa kijinsia katika jamii ili kuwapatia fursa wasichana kuendelea na masomo yao.

# TBS kujenga maabara Mwanza, Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limetaja vipaumbele saba kwa mwaka wa fedha 2022/23, ikiwamo kujenga maabara kwenye miji ya kimikakati ya Dodoma na Mwanza ili kusogeza huduma kwa wananchi.

Aidha, TBS ipo mbioni kupata kampuni za ukaguzi wa magari yanayotoka nchi za Uingereza, Dubai, Malaysia na Indonesia.

Akizungumza jana na waandishi wa habari Jijini hapa, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, alisema Shirika hilo limetenga Sh. bilioni 9.9 kwa ajili ya kujenga maabara hizo.

Alisema hatua hiyo italeta ufanisi katika utoaji majibu ya viwango vya bidhaa kwa wateja na kuondokana na kusubiri majibu kwa muda mrefu kutoka maabara iliyopo Dar es Salaam.

Pia, alisema Shirika limetenga Sh. bilioni 2.7 kwa ajili ya kuimarisha ofisi saba za kanda (Arusha, Mwanza, Mtwara, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma na Mbeya) pamoja na ofisi za mipakani, bandari za Tanga, Bagamoyo na Dar es Salaam, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Kambarage Nyerere.

"Lengo ni kuimarisha ukaguzi wa mara kwa mara sokoni ili kupunguza bidhaa hafifu sokoni na hatimaye kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa bora na salama," alisema.

Pia, alisema Sh. bilioni 1.6 zimetengwa kwa ajili ya kuandaa viwango 630 vya kitaifa katika sekta mbalimbali.

"Shirika limetenga Sh. bilioni 1.18 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ukaguzi wa bidhaa kabla ya kusafirishwa kuja nchini (PVoC) na baada ya kuwasili nchini ili kuhakikisha nchi haiwi jalala la kupokea bidhaa zilizopigwa marufuku au hafifu," alisema.

Akizungumzia ukaguzi wa magari, alisema kutokana na kulalamikiwa na wananchi kwasasa asilimia 97 ya magari yanayotoka Japan yanakaguliwa huko huko.

"Bado kuna zabuni tunamaliza ya magari yanayotoka nchi nyingine, zabuni tayari na karibu tutapata kampuni ambazo zitatusaidia kufanya kazi hiyo Uingereza, Dubai, Malaysia na Indonesia," alisema.

Kuhusu bidhaa za vipodozi vilivyokatazwa, Mkurugenzi huyo alisema vimekuwa vikiingia kwa njia mbalimbali za magendo ikiwamo kutumika kwa magari yanayobeba mafuta.

"Kuna wakati yamekamatwa magari yaliyopeleka mafuta ya dizeli nchi jirani, wakati wa kurudi wanaweka vipodozi vinakuja kutumika huku ni ngumu kidogo, lakini inawezekana kudhibiti," alisema.

Alishauri wanawake na wanaume wanaotumia vipodozi vilivyopigwa marufuku kuacha ili kulinda afya zao.

Pia, alisema wanaendelea kushirikiana na taasisi zingine kuangalia namna nzuri ya kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoagizwa mitandaoni.

Hata hivyo, kuhusu uwekaji vinasaba kwenye mafuta yanayotumika nchini, alisema Shirika hilo limeendelea kufanya kazi hiyo kwa ufanisi na kwasasa hakuna tatizo la uchakachuaji wa mafuta.




Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Charles Makongoro Nyerere (katikati), akizindua programu jumuishi ya taifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (PJT-MMMAM) katika mkoa huo mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Umeme joto ardhi kutatua changamoto vijijini

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SERIKALI imesema inawekeza nguvu kwenye uzalishaji wa umeme wa jotoardhi, kwa ajili ya kunufaisha wananchi wa maeneo ya vijiji na ambako kuna rasilimali hiyo tayari.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nishati, January Makamba, hivi karibuni wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Iramba, Kata ya Ntaba wilayani Rugwe mkoani Mbeya, baada ya kukagua miundombinu ya umeme wa jotoardhi.

Alisema serikali inaweka nguvu kwenye kuzalisha umeme kwa njia mbalimbali, zaidi kuvumbua vyanzo vipya kama jotoardhi ambayo ni nishati jadidifu na inahifadhi mazingira.

Kwa mujibu wa Makamba, katika bajeti ya mwaka huu, zimetengwa Shiling bilioni tano za kuendeleza miradi ya umeme wa joto ardhi na wamenunua mtambo maalum wa kuchoronga miamba kwa umbali wa kilomita tatu.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kufikia jotoardhi ambalo litatumika kuzalisha umeme na wamejiridhisha kuwapo vyanzo vingi vya kuzalisha nishati hiyo, kuliko umeme mwingine nchini.

"Ni muhimu kwenye Gridi yaTaifa kuwe na mchanganyiko stahiki ili chanzo kimoja kikileta shida labda mvua zikigoma kuwe na umeme wa chanzo kingine, jotoardhi haina hali ya hewa hii ni muda wote, tunategemea 2025 tutakuwa tumezalisha Megawati 200 kwa kuanzia, lakini mbele tunakoelekea tutazalisha zaidi," alisema Makamba.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA UTOAJI WA Curtain Bubble**
**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-EF-0002-00.**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, ununuzi na Ujenzi wa gati na Vifaa vya Kupakia mafuta ghafi kwenye Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni na wataalamu wenye uzoefu kueleza nia yao ya:

**Uundaji na Ugavi wa optimized Curtain Bubble.**
Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta ghafi yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo la Hifadhi ya Bahari lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga, nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA /HUDUMA:**
Sifa zinazopendekezwa za curtain Bubble ni:
- Urefu = m230,
- Umbali kutoka kwa chanzo cha sauti = m15,
- Bomba nje / kipenyo = mm40 / mm36,
- Compressor ya hewa = kiwango cha mtiririko cha 23 $m^3$ /dk (1380 $m^3$/saa) na shinikizo la chini la > bar 7
- Kipenyo cha mashimo kwenye hose ya curtain Bubble lazima iwe mm2;
- Nafasi ya mashimo kwenye pazia la Bubble lazima iwe sm10.

Ili kuongeza ufanisi wa Curtain Bubble. Mikengeuko (deviations) ya kiufundi inakubalika, ikiwa inathibitika na haizuii ufanisi wa curtain bubble (itategemea idhini ya BBJV) Mahitaji ya vifaa ni kama ifuatavyo:
- Mfumo 1 wa winchi wa futi 20,
- Bomba(hose) la curtain bubble m1 x 230,
- Mfumo 1 wa winchi wa ziada wa futi 20,
- Bomba (hose) la curtain Bubble la ziada la m1 x 230,
- Bomba (hose) 4 za usambazaji za mita 40,
- kontena la futi 20 lenye vipuri,
- Kpmpresa + 1 moja ya ziada

vifaa vya kuungia, kufungia na kupachikia mabmba (spooling devices)

**SIFA BAINIFU:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:
- Uwezekano wa kuwasilisha vifaa vyote vilivyoombwa kabla ya mwisho wa mwaka '22 katika bandari ya Tanga ,
- Rekodi inayofaa yenye uzoefu wa angalau miaka mitano (5) katika uundaji wa curtain bubbles,
- Wafanyakazi waliohitimu na kuthibitishwa kufanya kazi za Uthibiti Ubora / Uthibitishaji Ubora (QA/QC);
- Uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kufanya au kusimamia kandarasi husika.
- Alama ya CE,
- Ubora na mipango ya HSE na uthibitisho : ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018), EN ISO 14732, EN ISO 90606-1, ISO 11484, EN9-08 ISO 11484, EN9-8 ISO 18084 , 10893-11, au vyeti sawa;
- Kuzingatia kanuni za petroli na Matumizi ya rasilimaliza ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unashauriwa.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com; thomas.depauw@bbnjv.com (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **tarehe 16 Agosti 2022 , Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi vigezo yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na mkataba ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizokidhi matakwa ya awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa Wito wa Zabuni.

216972901

# Wadau biashara ya ngozi kujadili changamoto

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imesema imekutana na wadau wa ngozi kujadili changamoto na fursa zilizoko ili kuwanufaisha Watanzania kiuchumi.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Tixon Zunda, alisema hayo wakati wa ufunguzi wa mradi wa kukuza na kuendeleza sekta jumuishi ya ngozi nchi za Tanzania na Zimbabwe, utakaogharimu Sh. bilioni 1.1, kwa kushirikiana na Shirika la Solidaridad, unaotekelezwa kwa miaka miwili.

Alisema wizara hiyo ina wajibu wa kuhakikisha inapunguza na kuondoa vikwazo kwenye biashara ya ngozi ili kuongeza matajiri kupitia biashara hiyo.

"Kwa kipindi cha miezi sita, wizara imeshaondoa vikwazo, tozo na kodi 42, tunawaalika na nyinyi wadau kupitia halmashauri zenu, ikiwa kuna vikwazo, wekeni mezani nami nitayawasilisha ili yaweze kufanyiwa kazi, tunataka wafanyabiashara ya ngozi wawe matajiri kupitia biashara hii," alisema Zunda.

Alisema, ushirikiano huo utaisaidia serikali kupata kodi na wadau faida, ikiwa ni pamoja na kuzalisha ajira kwa vijana.

Wakati huo, alizitaka halmashauri hizo nchini kuwashirikisha vijana wa kike na kiume kwenye biashara ya ngozi ili kuleta tija.

"Bado ushiriki wa vijana na watu wenye mahitaji maalumu kwenye biashara ya ngozi ni mdogo, naagiza kupitia halmashauri zote nchini ikiwa ni pamoja na wadau wote kuona namna ya kuwajengea uwezo ili wapende kuifanya biashara hii," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shirika Solidaridad Tanzania, Mary Mkonyi, alisema mradi huo utasaidia kukabili matatizo ya kimazingira na kuongeza tija kwa kuyafikia masoko kwa urahisi zaidi.

Meneja mradi huo, Godlove Nderingo, alisema mradi huo utatumika kuelimisha wadau wa ngozi hasa wachakataji ili waweze kwenda kwenye teknolojia rafiki kwa mazingira.

Baadhi ya washiriki akiwamo, Paul Michael, alisema ipo haja kwa wizara kutambua ngozi ni dhahabu inayo tembea, kwa kuelimisha wachinjaji na wafugaji ili kupata ngozi bora.




Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Sahili Nyanzabara Geraruma, akiweka jiwe la msingi juzi kwenye mradi wa majisafi na salama katika kijiji cha Ididi Kata ya Nyamilangano Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama ambao utanufaisha wananchi 5,296 ambao unatekelezwa na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Kahama wenye thamani ya Sh. milioni 350. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mradi wa maji waleta neema Ushetu

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MBUNGE wa Jimbo la Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Emmanuel Charahani na madiwani wa wilaya hiyo, wamesema kukamilika kwa mradi wa majisafi na salama Kata ya Nyamilangano, kutapunguza adha ya kinamama kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Walibainisha hayo jana wakati kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Sahil Geraruma, alipofika kwenye uwekaji wa jiwe la msingi la upanuzi wa mradi wa maji Nyamilangano unaotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

"Namshukuru sana Rais kwa kuliangalia Jimbo langu kwa ukaribu zaidi, hapa tayari katika bajeti ya 2022/2023 ametupatia Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya maji," alisema.

Diwani wa Kata ya Nyamilangano, unakotekelezwa mradi huo, Robert Mihayo, alisema mradi huo utapunguza adha kwa kinamama kutembea umbali wa kilomita saba kwenda kisimani kuteka maji ambayo sio salama.

Naye Diwani wa Kata ya Igunda, Tabu Katoto, alisema serikali inawajali wananchi wake kwa vitendo na kuongeza kuwa licha ya upanuzi wa mradi huo wa maji, pia kwenye kata hiyo ambayo ndiyo makao makuu ya Halmashauri ya Ushetu, serikali imefanya mambo mengi muhimu.

Akisoma taarifa kwenye uwekaji wa jiwe la msingi, Mhandisi Magile Maduhu alisema, mpaka kukamilika kwa mradi huo utagharimu Sh. milioni 350 ambao umetekelezwa kwa kipindi cha miezi saba kwa mfumo wa Force Account na umeanza kipindi cha mwaka 2014.

Kwa upande wake kiongozi wa mbio za Mwenge, alisema mradi huo bado upo kwenye utekelezaji na kumtaka Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kutochelewesha mradi bila sababu za msingi.

"Natoa agizo ndani ya siku 14 mradi huo uwe umetekelezeka," aliagiza.

Mwenge huo unakwenda sabamba na ujumbe wa kaulimbiu isemayo "Sensa ni msingi wa mipango, shiriki kuhesabiwa tufikie malengo ya Taifa".

# Wakusanya taarifa sensa wapewa angalizo

**Na Pendo Thomas,** MWANZA

KAMATI ya ulinzi na usalama wilayani Magu, imesema itawachukulia hatua kali za kisheria wakusanyaji taarifa ya sensa ya watu na makazi watakaopoteza au kuharibu mali za serikali walizopewa pamoja na watakazokusanya tofauti na lengo lililokusudiwa.

Kauli hiyo, ilitolewa mwishoni mwa wiki wilayani Magu wakati wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ilipotembelea vituo vya mafunzo kwa wakusanyaji taarifa za sensa ya watu na makazi.

Akizungumza katika mafunzo ya makarani hao, Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, alisema mtu yeyote atakayebainika kupoteza mali ya serikali atahesabika amefanya makusudi kukwamisha ukusanyaji wa taarifa ya sense na atawajibishwa ipasavyo.

Aidha, Kali aliwaonya wakusanyaji wa taarifa kuacha 'kubumba' taarifa badala yake wafanye uhalisia ili taarifa zinazokusanywa ziwe na uhalisia ambao utaiwezesha serikali kutumia taarifa hizo katika uamuzi wa kimaendeleo.

Akizungumzia suala hilo, Kamanada wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, wilayani Magu, Gastone Tigulebwa alisema, hategemei kusikia kuna nyaraka au vifaa vimeungua na kila atakayekuwa na mali ya serikali anapaswa kuongeza umakini na kuepukana na mazingira hatarishi.

"Ni bora roho yako wewe ipotee, lakini kile kifaa cha serikali kipone, kwa hiyo sitegemei kusikia kuna moto umetokea kisha kifaa kikaungulia humo," alisema.

**Mtu yeyote atakayebainika kupoteza mali ya serikali atahesabika amefanya makusudi kukwamisha ukusanyaji wa taarifa ya sense na atawajibishwa ipasavyo.**

## Afungwa miaka 13 jela mauaji ya mpenzi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza imemhukumu Masunzu Bunzari (39), kifungo cha miaka 13 na miezi mitatu kwa kumuua mpenzi wake Sikora Manyanga kwa madai ya kumkuta na mwanaume mwingine chumbani.

Katika tukio hilo Bunzari anadaiwa kumuua bila kukusudia mpenzi wake kwa kumpiga nyundo kichwani, kumchoma kisu tumboni na utumbo kutoka nje.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, John Kahyoza, baada ya mshtakiwa kukiri kosa.

Awali akisoma maelezo ya mashtaka, Wakili wa Serikali, James Pallangyo, alidai mshtakiwa na marehemu Sikora walikuwa wapenzi, lakini mahusiano yao yaligubikwa na migogoro.

Alidai licha ya Sikora kuachana na mshtakiwa na kuendelea kumsihi warudiane, hakukubali ombi hilo jambo lililozidisha ugomvi wao.

Pallangio alidai kuwa Desemba mosi, mwaka 2018 majira ya usiku mshtakiwa alienda nyumbani kwa Sikora kwa lengo la kuomba warudiane.

Alidai kuwa aligonga mlango na alipoingia ndani alimkuta Sikora akiwa na mwanaume mwingine ndipo alipochukua nyundo aliyokuwa amekwenda nayo na kumpiga kichwani, alipoanguka alichomoa kisu na kumchoma tumboni hadi utumbo kutoka nje.

Wakili alidai, baada ya mshtakiwa kufanya ukatili huo alikwenda kijiji cha Shinyanga A, na kuchimba shimo ambalo alifukia nyundo na kisu hicho na kutokomea kusikojulikana.

Wakili Pallangio alidai kuwa asubuhi siku ya pili, majirani wa Sikora walipoona kimya bila kumuona walienda kufungua mlango na kumkuta akiwa kwenye dimbwi la damu.

Alidai kuwa, majirani hayo walitoa taarifa polisi ambao waliuchukua mwili huo. Aliendelea kudai kuwa chanzo cha kifo ni kuvuja damu nyingi na walimkamata mshtakiwa huyo ambaye alionyesha alikoficha silaha za jadi alizotumia.

Jaji Kahyoza alimuuliza mshtakiwa kama maelezo aliyoyasoma Wakili wa serikali yana ukweli na kukiri.

Jaji Kahyoza alimuuliza mshtakiwa alitumia nini kumuua mpenzi wake bila kukusudia na kujibu ni nyundo na kisu.

Mshtakiwa huyo alikuwa akitetewa na Wakili wa kujitegemea Penina Mashimba, ambaye alidai mteja wake ni mkosaji wa kwanza na amejutia kosa lake ndiyo maana amekiri kosa bila ya kulazimishwa.

Pia, alisema mteja wake alikaa mahabusu miaka minne na miezi minane ambayo amejifunza na kuiomba mahakamani hiyo kumpa mteja wake adhabu ndogo hasa ya kifungo cha nje.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali, aliiomba mahakama kutoa adhabu kwa kuwa uhusiano na marehemu ulishavunjika na hakua mkewe, hakupaswa kuwa na wivu naye.

Jaji Kahyoza alisema kitendo cha kupiga mtu nyundo kichwani mara nyingi na kuchukua kisu kumchoma tumboni hadi utumbo kutoka nje ni kitendo cha kikatili.

"Hivyo ninakuhukumu kwenda jela miaka 13 na miezi mitatu na muda uliokaa mahabusu gerezani upunguzwe na rufani ipo wazi kwa upande wowote ambao haujaridhika na hukumu hii," alisema Jaji.

# 'Unaweza kuwa na sukari, afya ya akili bila kujua'

**Na Joseph Mwendapole**

UGONJWA wa kisukari na tatizo la afya ya akili bila kujua huwapata watu kutokana na kutokuwa na tabia ya kupima afya mara kwa mara.

Hayo yamebainika kwenye kambi ya huduma ya ushauri, jijini Dar es Salaam.

Ugonjwa wa afya ya akili umeelezwa kuchangiwa na matatizo mengi ya ndoa, ajira, msongo wa mawazo, kutengana kwa wazazi na mawazo ya kujiua yaliyoshamiri kwa sasa nchini.

Mwanafunzi wa mwaka wa pili wa fani ya Ustawi wa Jamii katika Chuo cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), Jenice Mpanju, alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na Nipashe, wakati wa kufunga kambi ya mwezi mmoja ya kupima afya bure wananchi, iliyoandaliwa na Hospitali ya Kairuki Mikocheni na HKMU, maeneo ya Mlimani City.

Alisema katika kambi hiyo wamepima watu 615 na wengi waligunduliwa na tatizo la sukari na walipohojiwa ilibainika kwamba walikuwa hawajui wana ugonjwa huo.

Alisema miongoni mwa magonjwa waliyokuwa wakipima kwenye kambi hiyo ni sukari, shinikizo la damu, uwiano wa urefu na uzito na matatizo ya afya ya akili ambayo nayo yameonekana kuwa tatizo.

"Tatizo kubwa tulilogundua hapa ni watu kuwa na sukari, lakini hawajui kwamba wanashida hiyo. Pia wengi tumegundua wana shinikizo la damu, lakini tulipowahoji tulibaini kwamba wengi wanatambua hilo na wanaishi kwa kutumia dawa," alisema Jenice.

Kwenye kambi hiyo wanawake waliohudumiwa walikuwa 266 wakati wanaume ni 350, waliogunduliwa kuwa na tatizo walipewa ushauri wa kwenda kupata matibabu ya kibingwa kwa wataalamu wa afya.

Alisema kwenye huduma ya ushauri matatizo mengi waliyogundua ni ya ndoa, ajira, msongo wa mawazo, kutengana kwa wazazi na mawazo ya kujiua yaliyoshamiri kwa sasa.

"Tumebaini kuwa watu wengi wanaojiua wanakuwa wamekosa msaada wa ushauri nasaha wa nini wafanye na wapi waende wapate msaada sasa wakikosa hayo wanaamua kujiua kama suluhisho la shida zao, lakini wangewahiwa wasingejiua," alisema.

Alisema watu wengi bado hawajawa na mwako wa kwenda kupima afya zao mara kwa mara na kukumbusha kuwa kambi hiyo ya bure imekuwa msaada mkubwa kwao na kuahidi kuendelea kutoa huduma hiyo ya bure.

Kuhusu matatizo ya afya ya akili, Jenice alisema afya ya akili inachangiwa na vitu mbalimbali kama kutokula sawa sawa, kukosa utulivu kwenye familia, kukosa kazi, msongo wa mawazo na mifarakano.

"Watu wengi wakisikia tatizo la afya ya akili wanadhani ni kichaa wakati mtu anaweza kuonekana sawa, lakini akawa na tatizo sasa waliokuja hapa tumewaelezea viashiria vya mtu mwenye tatizo la afya ya akili," alisema.

Akizungumza kuhusu namna ya kumtambua mtu mwenye tatizo la afya ya akili, Jenice alisema huwezi kumtambua kwa kumtazama bali kwa namna anavyojitanabaisha mwenyewe kwako.

Alisema kwenye kambi hiyo zaidi ya watu 300 wamekubali kwamba wana tatizo la afya ya akili na kukubali kupata huduma ya kutibu tatizo hilo na wamechukua mawasiliano yao kwa ajili ya kuwasaidia kupata huduma zinazostahili.

Mkufunzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii (HKMU), Esther Katende, alisema waliamua kuandaa kambi hiyo ya bure ya mwezi mmoja baada ya kubaini kuongezeka kwa tatizo la afya ya akili kwenye jamii kunakosababisha wengi kujiua na kuua wengine.



Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Bonde la Kati, William Mabula, akionyesha zana za kazi baada ya kukabidhiwa na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alipozindua bodi hiyo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## Maabara ya kisasa kusogezea huduma wananchi Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama imetenga Sh. milioni 803.4 na kuanzisha ujenzi wa maabara ya kisasa itakayopima magonjwa makubwa na madogo ili kuwasogezea wananchi huduma.

Wagonjwa kwa sasa wanalazimika kusafiri kupata huduma ya vipimo katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando, KCMC na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Fedha hizo zinatokana na mapato ya ndani ya halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na huduma zitakazokuwa zikitolewa ni pamoja na X-Ray, Ultra Sound, CT- Scan na utoaji wa damu ili iendelee kuwasaidia waliopata ajali au wajawazito.

Mganga Mkuu wa Manispaa hiyo, Dk. Josephat Shani, aliyabainisha hayo juzi wakati akitoa taarifa ya ujenzi wa maabara hiyo mbele ya kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa mwaka 2022, Sahil Nyanzabara.

Alisema, ujenzi huo ulianza Februari 14, mwaka huu na unatarajia kukamilika Novemba mwakani.

Alisema halmashauri hiyo imetenga Sh. milioni 803.4 na kati ya hizo Sh. milioni 500 zimetoka serikali kuu na Sh. milioni 303.4 ni fedha kutoka mapato ya ndani ya manispaa hiyo na mpaka sasa wameshatoa Sh. milioni 330.1 kwa ajili ya kulipa mkandarasi anayejenga jengo hilo kampuni ya Suma JKT.

"Kipindi cha hayati Dk. John Magufuli alitupatia fedha Sh. milioni 500 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) kwa kuwa fedha za ukamilishaji tulikuwa nazo tukaona fedha hizi tuzitumie kujenga maabara ya kisasa," alisema Dk. Shani.

Alisema halmashauri hiyo imenunua magari mawili ya dharura ya wagonjwa kwa Sh. milioni 272.7 ambazo ni mapato ya ndani, kabla ya ununuzi wa magari hayo gari lililokuwa linatumika kubeba wagonjwa lilikuwa moja.

Kwa upande wake, kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Nyanzabara alisema ameridhishwa na ujenzi wa maabara hiyo unavyoendelea na kuwataka Suma JKT kukamilisha kwa muda uliopangwa ili kuanza kutoa huduma kwa wananchi wanaofika hospitali kutibiwa.

Aidha, aliitaka ofisi ya ununuzi ya manispaa, Ofisa ya Mkurugezi na Suma JKT kuwa na vielelezo vya malipo yanayofanyika kipindi cha ujenzi.

Alisema amebaini malipo hayana vielelezo wala stakabadhi zinavyoonyesha yamefanyika kwa Suma JKT.

"Tukumbuke kila malipo yanayofanyika lazima halmashauri ipate stakabadhi ya malipo au barua ya kukiri kupokea fedha kutoka Suma JKT na sio kulipa malipo bila kupata vielelezo, rekebisheni hii dosari iliyoko na niwapongeze kwa ujenzi huu," aliongeza Nyanzabara.

Kuhusu ununuzi wa magari mawili ya dharura ya wagonjwa, Nyanzabara alitaka halmashauri kuyatumia katika kazi iliyokusudiwa na hategemei kusikia siku zijazo yamekamatwa yakihusishwa na vitendo viovu.

# DC: Sensa itarahisisha ugawaji rasilimali sawa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, amesema mgawanyo wa rasilimali hauko sawa kutokana na kutokuwa na takwimu sahihi ya watu, huku akiwataka wananchi kujitokeza kuhesabiwa kuiwezesha serikali kupanga mikakati.

Akizungumza jana na viongozi wa madereva bodaboda, viongozi wa soko na wasafirishaji wa daladala katika kikao cha kujadili namna ya kuhamasisha watu kushiriki sensa, mjini Mlandizi, alisema ushiriki wa kila Mtanzania ni muhimu kwa manufaa yake na taifa kwa ujumla.

Alisema ili mgawanyo uende sawa na kila mmoja apate huduma stahiki ni vyema wananchi washiriki kuhesabiwa Agosti 23, mwaka huu, na kwamba ni muhimu kwa serikali ili iweze kupeleka huduma inayoendana na idadi ya watu.

"Rais amewekeza kwenye anwani za makazi na sensa ya watu wananchi tutoe ushirikiano kwa makarani wa sensa, nimewaita nyie, ili mnisaidie kuhamasisha na wataalamu wataendelea kutoa elimu kila mahali kuhusiana na umuhimu wa hili jambo," alisema.

Kadhalika, Msafiri aliwataka wafugaji kuondokana na dhana mifugo ikihesabiwa inakufa badala yake waruhusu ili dawa ziweze kutolewa za kutosheleza idadi iliyoko.

Alimwelekeza Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Kibaha kuitisha kikao cha wanawake ili wapewe elimu ya sensa na kwamba kutokana na ushawishi wao wataisaidia jamii kujitokeza kwa wingi.

Kwa upande wake, Mratibu wa Sensa wa halmashauri hiyo, Gele Msangi, aliwataka wananchi kuzingatia kutoa taarifa sahihi kwa makarani wa sensa.




Mwezeshaji wa shughuli ya uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha na kutoa elimu ya chanjo ya UVIKO -19, iitwayo 'Tanzania Iko Tayari', Redmptus Caesar, akizungumza katika uzinduzi huo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watanzania kufikia asilimia 70 chanjo UVIKO

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wametakiwa kuendelea kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kufikisha malengo ya kitaifa ya utoaji chanjo ya ugonjwa kwa asilimia 70 ifikapo Desemba, mwaka huu.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam juzi na Mratibu wa Uelimishaji na Uhamasishaji Jamii toka Wizara ya Afya, Peter Mabwe, alipokuwa akizindua kampeni ya kutoa elimu na kuhamasisha chanjo iitwayo 'Tanzania iko Tayari'.

Kampeni hizo zinatarajiwa kufanywa kwa pamoja na taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali ikiwamo Africa Union, Access Challenge, African CDC, Jakaya Kikwete Foundation na Clouds Media Group (CMG).

"Malengo ya kitaifa ya utoaji chanjo ni kufikia asilimia 70 ya walengwa wote ambao ni Watanzania wa umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea ili ifikapo Desemba mwaka huu wawe wamechanjwa," alisema Mabwe.

Alisema jambo la muhimu kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa jamii kwa kuzingatia ainisho la makundi yaliyo katika hatari zaidi kuhusu UVIKO-19 na kuona namna ya kuhakikisha ujumbe wa uelimishaji unaoandaliwa unawafikia na kuwagusa wananchi.

Wataalamu wa Wizara ya Afya watashirikiana wadau wengine katika kampeni hiyo ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa na kufikia asilimia 70 ya Watanzania waliochanjwa yanatimia.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa nchi inakuwa salama dhidi ya magonjwa na dharura mbalimbali za kiafya na kwamba ili kufikia azma hiyo ni muhimu wananchi wapate taarifa sahihi na kwa wakati.

"Elimu sahihi ni muhimu ili kuepusha upotoshaji unaojitokeza kuhusu UVIKO-19 na dharura nyingine za kiafya ikiwamo wasiwasi wa hatua zinazochukuliwa kudhibiti mangonjwa haya," alisema.

Alitoa mfano jinsi Watanzania walivyoonyesha wasiwasi kuhusu chanjo dhidi ya UVIKO-19 katika hatua za mwanzo za utoaji chanjo na kusababisha mwitikio wa matumizi ya chanjo kuwa hafifu.

"Kama ilivyo kwa nchi nyingine, Tanzania imeendelea kuhakikisha mikakati madhubuti ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo ikiwamo utoaji wa chanjo inatekelezwa ili kuifanya jamii kuwa salama na kupunguza athari kwenye shughuli za maendeleo na kiuchumi nchini na duniani," alisema.

Mratibu wa Kampeni ya Tanzania iko Tayari Ben Mcharo alisema, baada ya uzinduzi huo, wanasubiri kupangiwa na mikoa na Wizara ya Afya ili waende kuhamasisha jamii kujitokeza kwa wingi kupata chanjo.

"Tunataka kwenda kwenye mikoa ambayo bado iko chini katika uchanjaji, kuongeza nguvu ya kuhamasisha na kutoa elimu wananchi waelewe umuhimu wa chanjo ili wajitokeze kwa wingi kupata huduma hiyo," alisema Mcharo.

Alifafanua kuwa, wataendesha kampeni hiyo wakiambatana na wataalamu wa afya kutoka Shirika la FH360, ambao kazi yao itakuwa ni kuchanja Watanzania watakaokuwa tayari kufanya hivyo.

Hivi karibuni, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alikaririwa na vyombo vya habari akitoa takwimu za watu waliochanjwa na kufafanua kuwa hadi kufikia Julai 18 mwaka huu, watu milioni 11.4 wamepata dozi kamili, kati ya watu milioni 30.7 ambao serikali imewalenga.

# Benki ya Mkombozi yapata faida bil. 3/-

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya Biashara ya Mkombozi kwa mwaka 2021 imepata faida ya Shilingi bilioni tatu kutokana na ufanisi wa kiutendaji na matokeo chanya ya utekelezaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Gasper Njuu, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano mkuu wa 13 wa wanahisa uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Njuu alisema Benki ya Mkombozi ilipata matokeo ya kuridhisha katika vigezo muhimu vya mizania ya viwango vya upatikanaji wa faida.

"Benki ilipata faida ya kuvutia na ubora katika ujenzi wa mtaji uliochangiwa na ufanisi wa kiutendaji wa biashara na matokeo chanya ya utekelezaji mikakati mbalimbali ya maendeleo," alisema.

"Tulijikita katika fursa za ukuaji wakati tukichukua hatua chanya kukabiliana na matatizo yaliyokuwapo katika mazingira yetu ya kiutendaji."

Njuu alisema licha ya matatizo mbalimbali yaliyojitokeza mwaka 2021, benki inaendelea kujikita kimkakati kupanua mawasiliano na wateja kupitia huduma za mawakala, vituo vidogo vya huduma za kibenki chini ya matawi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Mkombozi, Respige Kimati, alisema utendaji wa benki hiyo kwa mwaka huu umewekwa katika hali njema ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Kimati alisema matarajio ya benki hiyo yanahitaji mtaji endelevu, hususani kwa kuingiza mtaji mpya ili kusaidia uwekezaji muhimu na ukuaji wa mizania.

"Wito wetu kwa wanahisa ni kuendelea kuunga mkono mipango ya uwekezaji wa benki katika azma hii ili kutoa matokeo yenye faida, thabiti na endelevu kwa benki. Baada ya kupita awamu ya miaka mitatu ya mabadiliko ya biashara na kujipanga," alisema Kimati.

Alisema benki iliongeza fedha za wanahisa kwa asilimia 26 hadi kufikia Sh. bilioni 25.8 kutoka Sh. bilioni 20.5 za mwaka uliotangulia.

Alisema ukuaji huo umechangiwa na kuingizwa kwa mtaji nyongeza ya Sh. bilioni 2.2 na faida ya mwaka iliyowekezwa.

Uwiano wa mtaji, alisema ulikuwa Sh. milioni 19.5 wenye mnyambulisho wa asilimia 14.63, ukilinganishwa na wa mtaji wa Sh. milioni 16.4 wenye unyambulisho wa asilimia 11.08 kwa mwaka 2020.

Alisema mtaji wa benki upo juu ya mtaji unaotakiwa kisheria wa Sh. bilioni 15.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 2, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 13

## LINDA MZINGIRA (3) Bila misitu hii mamlaka za maji kuwa hoi




Ukurasa 12

## CHORA RAMANI Kampeni ya kutafakari kwanza inayopambana na ukatili kijinsia

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Homa ya ini inavyofanana na UKIMWI

■ Kujamiiana, sindano, nyembe vyanzo

JULAI 28, 2022 dunia inaadhimisha Siku ya Homa ya Ini inayolenga kuwakumbusha na kuwajengea uelewa wanajamii kuhusu ugonjwa huo unaoshambulia ini kwa kasi na na kulikwamisha kufanya kazi yake kikamilifu.

Homa ya ini ni ugonjwa unaosababisha ini kuvimba mara nyingi unatokana na virusi viitwavyo 'hepatitis C'.

Aidha, huletwa na madhara ya sumu mbalimbali, mfano, pombe, dawa, kemikali na maambukizi mingine na maradhi yanayochochewa na kingamwili (Autoimmune disease) inayotokea pale kinga ya mwili ambayo ilikuwa na jukumu la kuuzuia mwili na maradhi, inabadilika na kuanza kushambulia seli zinazoukinga na magonjwa.

Mwaka huu kauli mbiu ni kufikia utokomezaji wa homa ya ini ndani ya mifumo ya afya inayoendelea.

Kwa mujibu wa Mtandao wa Habari za UN News, Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria kuwa asilimia 90 ya watu huishi na ugonjwa huo wa ini bila kujitambua, huku takribani watu 3,000 wakifariki dunia kila siku kutokana na kusumbuliwa na maradhi ya homa ya ini aina hepatitis B na C.

Hata hivyo, kila baada ya sekunde 30 mtu mmoja hupoteza maisha kutokana na maradhi hayo, hatua ambayo mashirika ya afya duniani, serikali na taasisi zisizo za kiraia kuanza kutoa elimu kwa jamii wakihamasisha watu wapime ili kupata chanjo na kutibu homa ya ini.

Ni nia ya WHO kuutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030 na kutoa wito kwa nchi kufikia malengo mahususi ili kupunguza maambukizi mapya ya hepatitis B na C kwa asilimia 90, UN News inasema.

Aidha, inalenga kupunguza vifo vinavyohusiana na homa ya ini na saratani kwa asilimia 65 kwa kuhakikisha kuwa angalau asilimia 90 ya watu walio na virusi vya hepatitis B na C wametambuliwa na kutibiwa.

### KUAMBUKIZWA

Daktari mbobezi wa magonjwa ya ndani (internal medicine) Dk. Joseph Pantaleo, anazungumza na Nipashe kuhusu hali ya homa ya ini nchini, akiangazia maambukizo.



Dalili ya homa ya ini ni rangi ya ngozi, viganja na macho kuwa manjano. **PICHA: MTANDAO**

Anasema zipo njia mbalimbali kama uambukizo kutoka mtu kwenda kwa mtu mfano, mwenye maradhi hayo anaweza kumwambukiza mtu mwingine iwapo atashika damu au maji maji za mwili wake kupitia kidonda au mchubuko mwilini.

Aidha, Dk. Pantaleo anasema mjamzito anaweza kumwambukiza mtoto wake aliye tumboni kupitia michakato ya kujifungua.

Anataja pia suala la matibabu iwapo utaongezewa damu ambayo haikupimwa kikamilifu yenye virusi vya homa ya ini unapata maradhi hayo.

"Kujidunga sindino kwa wanaotumia dawa za kulevya au kujamiiana mke na mume au ngono za jinsia moja iwapo mmojawapo ana ugonjwa huo anaweza kumwambukiza mwenzake" anasema Dk. Pantaleo.

Anaeleza kuwa wakati mwingine watu wanaweza kuambukizwa kupitia kuchomwa sindano au kutibiwa na vifaa tiba ambavyo havikutakaswa, mfano kuchomwa kwa uzembe sindano ambayo ina damu ya mtu mwenye virusi kunaweza kueneza maradhi kwa mgonjwa ambaye awali alikuwa hana maradhi hayo.

Lakini anawataja wahudumu wa afya hospitalini ambao wanaweza kuambukizwa wakitoa matibabu kwa wagonjwa waliathirika na homa ya ini.

Akizungumzia waathirika anasema kundi mojawapo ni wanawake wajawazito na watoto walio tumboni, wagonjwa wa UKIMWI ambao kinga ya mwili imedhoofika, wafanyakazi kwenye huduma za afya.

Walioongezwa damu ni kundi jingine ambalo linaweza kuathirika endapo wakati wa kulishwa damu hiyo, haikupimwa virusi vya homa ya ini, anaongeza.

Anawataja wanaoshiriki ngono za jinsia moja kuwa wapo kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa ugonjwa huo pamoja na wanaotumia dawa za kulevya kwa kujidunga sindano inayochangiwa na kundi kubwa la watu.

### HALI ILIVYO

Dk. Pantaleo anayefanyakazi katika Hospitali ya Mwananyamala Dar es Salaam, anasema kuwa Jiji la Dar es Salaam, lina kiwango kikubwa cha maambukizi ikiwa ni asilimia 7.2.

Anafafanua kuwa katika kila wagonjwa 100 saba wanaweza kugundulika na homa ya ini, wakati katika wagonjwa 1,000 takribani 72 wanakutwa na virusi hivyo.

Anasema njia pekee ya kujitambua na kuwa salama ni kupima na kuchunguzwa afya kama umeathirika unatibiwa, kama bado unapewa chanjo.

AINA ZA VIRUSI

Mtandao wa Habari za Umoja wa Mataifa -UN News, unamkariri daktari mbobezi wa magonjwa ya mfumo wa chakula wa Hospi-

INAENDELEA UK. 14

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

## CHORA RAMANI

# Kampeni ya kutafakari kwanza inayopambana na ukatili kijinsia

KITUO cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam, kimekuja na kampeni inayoitwa 'Chora Ramani', ikiwa na lengo la kutoa elimu na kuijengea jamii uwezo na mbinu mbalimbali zikiwamo za kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Sauti ya Jamii inaamini kuwa elimu hiyo itakuwa msaada mkubwa ndani ya jamii, iwapo itasambaa nchi nzima, hasa kutokana na vitendo hivyo kuripotiwa kutokea maeneo mbalimbali ya Tanzania.

Selemani Bishagazi ni Mkurugenzi wa kituo hicho kinachohamasisha vita kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia anafafanua zaidi kuhusu utoaji wa elimu hiyo alipozungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam juzi.

"Lengo la kampeni ya 'Chora Ramani', ni kutaka kuhakikisha kila mtu kwa nafasi yake kabla ya kufanya jambo lolote, anachora ramani kwa kutafakari ili imsaidie kujua kile anachojiandaa kukifanya," anasema.

Bishagazi anasema anatakiwa kutafakari kwanza na kufanya uchambuzi kabla ya kutenda jambo na kwamba hatua hiyo itamsaidia kuonyesha matokeo ya kile anachokusudia kukifanya.

Anasema wanawafundisha watu jinsi ya kutambua vitendo vya ukatili na kuviripoti sehemu polisi, serikali za mitaani na kwa viongozi mbalimbali kwa hatua za kisheria.

"Unajua kumtukana mtu bila kosa, kutompeleka shule, kukeketa na mambo mengine ya aina hiyo ni ukatili, lakini jamii inaweza kuona kama ni mambo ya kawaida, hivyo tunaelimisha ijue hilo," anasema.

Anaongeza kuwa mtu anaweza ana matarajio fulani katika maisha yake, lakini asijue jinsi ya kuyafikia, na kwamba wanamfundisha mbinu mbalimbali za kuweza kufika kule alikosudia.

"Vilevile watoto wanaweza kuwa na vipaji ambavyo vinatakiwa kuendelezwa, lakini wazazi wasitambue hilo, hivyo tunawagusa wa kuwaelimisha jinsi kuibua vipaji vya watoto wao," anasema.

Anafafanua kuwa mtoto anaweza kuwa na ubunifu wa kitu, lakini wazazi au walezi wasimwendeleze na kwamba kupitia kampeni hiyo anaamini itakuwa rahisi kuvitambua na kuviendeleza.

Mkurugenzi huyo anaongeza kuwa kampeni hiyo pia itasaidia jamii kuchora ramani itakayoonyesha faida za kila mtu kushiriki katika kuzuia vya ukatili na kujengea uwezo vikundi na watu binafsi njia ya kupita na kufikia malengo.

### KINACHOFANYIKA

Anafafanua kuwa kampeni hiyo inaendeshwa na vikundi vilivyoko kwenye jamii, mitandao ya kijamii, redio, magazeti na televisheni, viongozi wa dini na wa vyama vya siasa huku kituo hicho kikiratibu.

Bishagazi aliwataja wadau wengine katika kampeni hiyo ilioanza baada ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika kuwa ni Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).

Anasema hadi sasa wameshafika katika kata za Mzinga, Majohe, Kimara, Kipunguni na Msongola mkoani Dar es Salaam, wanaendelea na maeneo mengine, lengo letu likiwa ni kuhakikisha kampeni inafika nchi nzima.

"Tunaendelea kutoa elimu hii mkoani Dar es Salaam, lakini nifafanue kuwa tupokwenda kwenye vyombo vya habari na kuizungumzia, ni wazi kwamba tunakuwa tumeifikisha nchi nzima," anasema.

Anasema ndani ya jamii wapo baadhi ya watu ambao hawakubahatika kupata elimu ya darasani na wengine wameipata, lakini wanaweza kuwa ni wakatili, na kwamba kupitia kampeni hiyo wanaweza kubadilika.




Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Seleman Bishagazi (mwenye fulana nyekundu), akiendesha moja ya kampeni ya 'Chora Ramani'. P**ICHA: SABATO KASIKA**

"Tunaamini kwamba kupitia kampeni hii, jamii nzima wakiwamo wasomi na wasio wasomi, kila mmoja atajitafakari na kuchora ramani ambayo itamwezesha kutimiza malengo yake na ya watoto wake," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema ni muhimu kufahamu masuala yanayohusu ukatili na unyanyasaji wa kijinsia na kuyatafutia ufumbuzi kwa pamoja, ili hatimaye kuwa na jamii inayothamini utu wa mtu.

### NI WAKATI MWAFAKA

Kiongozi wa vijana Mtaa wa Nzasa Kimara, Asha Msango anasema, kampeni hiyo imekuja wakati mwafaka wakati huu ambao baadhi ya watu wamekuwa maamuzi ya kufanya vitendo vya ukatili bila kujipa muda wa kutafakari.

Anasema kila kukicha yamekuwa yakiripotiwa matukio ya watu kujichukulia sheria mkononi na kuondoa uhai wa wenzao, ikiwamo mume kuua mke, mke kuua mume, watoto wa kike kukeketwa na mengine mengi.

Msango anaongeza kuwa katika mazingira hayo, jamii haina budi kupata elimu ambayo itaisadia kuondokana na matendo hayo ya kikatili ambayo hayapaswi kufanywa na jamii iliyostarabika.

"Ni imani yangu kwamba, watu wataizingatia elimu hii inayotolewa, ili iweze kuleta matokeo chanya, hasa kwa upande wa vitendo vya ukatili katika jamii, ambavyo vimekuwa vikiongezeka kila kukicha," anasema Msango.

Sea Temba ni kiongozi wa vikundi vya vikoba kutoka Kata ya Majohe, anasema kuna haja ya watu kuwa na hofu ya Mungu ili kujiepusha na ukatili wa aina yoyote, badala ya kuwaogopa binadamu.

Anasema, serikali imekuwa ikiandaa mikakati mbalimbali ikiwamo kuanzisha MTAKUWWA, ili kutokomeza vitendo vya ukatili na kwamba kampeni ya 'Chora Ramani' inafaa kila eneo na itakuwa na mchango mkubwa.

### HALI YA UKATILI NCHINI

Takwimu za mwaka 2021 zinaonyesha kuwa watoto 11,950 walifanyiwa vitendo vya ukatili, 5,899 wakiwa wamebakwa, 1,114 kulawitiwa ambapo wa makadirio ya serikali ni asilimia 12 ya vitendo ndivyo vimeripotiwa.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima anatoa takwimu hizo katika mkutano wake na waaandishi wa habari jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

Alikuwa akifafanua majukumu ya wizara hiyo na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 na kufafanua kuwa vitendo vya ukatili vimeendelea kuongezeka katika jamii.

"Mwaka 2021 watoto 1,114 walilawitiwa, hii ni watoto 93 kwa mwezi. Asilimia 60 ya vitendo hivi hufanyika majumbani ambako wanafamilia ndio wahusika, huku asilimia 40 vikifanyika shuleni," anasema Dk. Gwajima.

Aidha, anasema serikali imekuja na mikakati mbalimbali ya kukomesha vitendo hivyo, mojawapo ikiwa ani uanzishwaji wa madawati ya ulinzi na usalama kwa mtoto ndani na nje ya shule na mabazara yao ili kuwashirikisha kujalidili masuala yanayowahusu.

ELIMU

NA DK FELICIAN B. KILAHAMA

## LINDA MZINGIRA (3)

# Bila misitu hii mamlaka za maji kuwa hoi

## •Imo Uluguru, Usambara Mashariki, Gairo




Viongozi wa serikali wakikagua maji katika chanzo cha Ruvu Chini mkoani Dar es Salaam. Uhai wa Mto Ruvu ni misitu ya Uluguru iliyoko mkoani Morogoro. **PICHA: MTANDAO**

KATIKA makala ya Jumanne iliyopita suala la umuhimu wa miti au misitu kwa sekta za kilimo na mifugo, lilichambuliwa kwa kina na kuonyesha kuwa misitu ni mali na katika andiko hili tunaiangalia thamani ya misitu kwenye sekta ya maji.

Katika vitabu vya Mungu suala la kuumba maji linatajwa "Mungu aliziumba mbingu na nchi,nayo nchi ilikuwa tupu, tena bila umbo na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji,Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji" (Mwanzo 1:1-2). Haya yalitokea siku ya kwanza kati ya siku sita Mungu alizofanya kazi kubwa kwa vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana.

Kwa hali hiyo rasilimali maji ilikuwa kati ya vitu vya kwanza kuwekwa duniani ikiwa ni pamoja na mbingu na nchi, yanachukua sura tofauti ikiwamo maji yenye chumvi katika bahari na sehemu za nchi kavu.

Yapo yasiyokuwa na chumvi au ya baridi kwenye nchi kama mito, mikondo, pamoja na mabwawa, mengine yapo chini ya ardhi ya chumvi na yasiyo na chumvi na pia yapo angani katika hali ya mvuke na mawingu.

Kupitia mvuke na mawingu tunapata mvua au ukungu kufuatana na majira kiini cha makala hii ni uhusiano wa maji na misitu.

Misitu na maji ni rasilimali zinazotegemeana kwa kiasi kikubwa, maji huwezesha uoto wa asili ikiwa ni pamoja na mimea, miti, misitu ya asili na mashamba ya miti ya kupanda katika sehemu za makazi kuweza kuota na kustawi.

Ili misitu na uoto wa asili uwepo na uendelee kustawi lazima yawepo maji au unyevunyevu ardhini. Mwenyezi Mungu alilijua hili ndiyo maana akaweka maji mwanzo kabisa, siku ya kwanza ya uumbaji wake.

Kwa hali hiyo, ni vyema tukafahamu maji yanatoka wapi na uhusiano wake na misitu ukoje. Cha muhimu ni kwamba maji yanayotumika kila siku katika nyumba zetu, iwe ni kupikia chakula, kusafishia vyombo, kufua na kuoga hata kumwagilia bustani na kilimo cha mboga yanatolewa kwenye mito kama Mto Ruvu na mto Wami unaonufaisha wakazi wa Dar-es-Salaam na sehemu kadhaa za mikoa ya Pwani na Morogoro.

Kwa Mamlaka za maji safi na maji-taka mfano, DAWASA kwa Dar-es-Salaam na Pwani wanatoa maji kupitia vyanzo vyake sehemu za Mto Ruvu kwenye matekeo (intake) za Ruvu Juu na Ruvu Chini.

Vilevile, kuna maji chini ya ardhi ambayo ili watu wayatumie lazima kuchimba visima. Isitoshe tunaweza kupata maji kutoka kwenye mabwawa na wakati mwingine huvuna maji ya mvua na kuyahifadhi kwa matumizi ya nyumbani.

Kwa wanaosafiri kupitia barabara ya Morogoro, ukifika eneo la Ruvu Darajani utaona Mto Ruvu. Wanaopita barabara ya Bagamoyo watauona sehemu za Bagamoyo kabla haujaingiza maji baharini.

Tanzania ina mito mingi mikubwa na midogo na karibu yote vyanzo vyake ni katika misitu ya asili, ambayo hujulikana kama misitu-lindimaji (swamp forests).

Hii ni muhimu katika nchi hii, ukiacha suala la maji ni maeneo yenye kuhifadhi bioanuwai ambazo ni aina kadhaa za mimea na wanyama wasiopatikana sehemu nyingine duniani isipokuwa hapa nchini pekee.

Hivyo, maeneo hayo ya misitu ni muhimu sana kitaifa na kidunia. Mito mingi nchini vyanzo vyake ni katika misitu ya aina hiyo mathalani, Mto Ruvu chanzo chake kikuu ni misitu ya asili katika Milima ya Uluguru mkoani Morogoro. Unapopanda mlima kuelekea Mvuha, mwanzoni mwa msitu wa Uluguru, utaona mto ukitokea msituni ukiwa umesheni maji mengi yakiwa safi bila tope na uchafu mwingine.

Vilevile, msitu huo unatoa vijito vingi kupeleka maji kwenye Bwawa la Mindu, Manispaa ya Morogoro na mingine kuingiza maji Ruvu. Mito mingine mikubwa ni pamoja na Mto Zigi (Sigi) wenye vyanzo vyake katika misitu iliyopo Milima ya Usambara Mashariki.

Mto huu unategemewa sana na wakazi wa Jiji la Tanga kama chazo chao muhimu cha maji. Ukibahatika kutembelea hifadhi mazingira asilia ukitokea Muheza na unapoanza eneo la hifadhi utaona Mto Zigi ukiporomosha maji kutoka kwenye misitu.

Mito mingine ni Mto Wami wenye vyanzo vyake katika misitu ya Ukaguru, Gairo na Rubeho, maji yake hutumiwa na watu wengi mkoani Morogoro na Pwani hasa maeneo ya Chalinze na viunga vyake , aidha maji yake ndiyo yanayonyewa na wakazi wengi wa mkoa wa Pwani.

Kuna Mto Pangani ambao huwanufaisha wakazi wa Wilaya za Same, Korogwe, Muheza na maeneo mengineyo ya mkoa wa Tanga. Vyanzo vya Pangani ni misitu ya Milima ya Usambara Magharibi, misitu katika milima ya Pare Kusini na Kaskazini pamoja na misitu ya maeneo ya Kilimanjaro.

Kwa sehemu za Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania kuna Mto Kihansi ambao huanzia katika misitu ya Kihansi ambapo kuna vyura vya aina yake kwa dunia nzima wanapatikana Kihansi pekee.

Mto Ruaha Mkuu vyanzo vyake ni misitu katika milima mkoani Mbeya, pia misitu katika eneo la Kilombero mfano, kwenye milima ya Udzungwa na Ukwiva. Mto Ruaha Mdogo ambao maji yake huingia Ruaha Mkuu (Great Ruaha River) huanzia kwenye ukanda wa Iringa ukiunganishwa na shamba la miti, Sao-Hill na maeneo ya misitu ya Hifadhi Asilia za Kilombero na Udzungwa Scarp.

Vilevile, katika maeneo hayo ya misitu huanzia Mto Kilombero ambao pia huungana na Ruaha Mkuu na kufanya Mto Rufiji ambao huwanufaisha wananchi wengi katika mkoa wa Morogoro na Pwani hasa umwagiliaji kilimo cha miwa na mpunga.

Kadhalika, misitu katika milima ya mikoa ya Mbeya, Njombe, Ruvuma ni vyanzo kwa Mto Ruvuma ambao pia unamanufaa makubwa kwa wananchi wa maeneo hayo.

Nimeonyesha baadhi ya mito michache lakini ipo mingi kama Mto Malagalasi auMoyowosi, Mto Mara, Mto Kagera, Mto Ngono na Mto Ruhuhu.

Katika Makala ijayo, nitafafanua jinsi misitu inavyochangia mito niliyotaja katika makala hii kutiririsha maji na kuchangia ustawi wa maisha ya Watanzania.

Vilevile, tukifikia hatua hiyo migogoro na uhasama kati ya wakulima na wafugaji vitapotea hivyo hali kuwa shwari kwa faida ya wote.

ELIMU

# Homa ya ini inavyofanana na UKIMWI

INATOKA UK. 11

tali ya Bugando mkoani Mwanza, David Majinge, akisema ugonjwa huo wa homa ya ini unasababishwa na virusi vya hepatitis C waliogawanyika katika makundi matano ambayo ni hepatitis A, B, C, D, na E.

"A na E huambukiza zaidi kwa njia ya chakula, kama umekula chakula kilichochafuliwa au vinywaji ambavyo vina 'contamina.

Ni vyakula au vinywaji vilivyochafuliwa na kinyesi ndivyo vyenye ugonjwa huo na mara nyingi kwa kuzingatia usafi wa chakula, watu wanaweza kujikinga wasipate maambukizi ya homa ya ini ambayo ni A na E", anasema Dk. Majinge.

Hata hivyo aina hiyo hupona na haina athari kubwa kama ile ya virusi vya B au C.

Aina nyingine za virusi vya hepatitis B, C, na D huambukizwa kwa njia ya kugusana kwa maji maji ya mwilini kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine. Mfano damu na ute wakati wa kujamiiana.

"Homa ya ini kama ilivyo kwa ugonjwa kama UKIMWI, ukishika damu ambayo ina maambukizo, majimaji ya njia ya uke kwenye kujamiiana pia inaweza kukuambukiza," anasema Dk. Majinge.

Anawazungumzia wanaotumia dawa za kulevya kwenye kujidunga kama wanachangia vitu vyenye ncha kama sindano, mswaki, nyembe au unapoenda kupata huduma katika sehemu ambazo hazizingatii usafi unakuwa uko katika hatari ya kuambukizwa," anaongeza Dk. Majinge.



Kuchangia sindano na viwembe kwa waganga na kwenye dawa za kulevya kunaweza pia kuambukiza homa ya ini . **PICHA: MTANDAO.**

Anasema watu wanaweza kujikinga kwa kuacha kutumia dawa za kulevya zikiwamo za kujidunga lakini ni vyema kujiepusha na kuchorwa michoro ya kwenye ngozi au 'tatuu'.

Anasema ni hatari pia kutoboa masikio kwa masonara ambao hufahamu usafi wa vifaa vyao na lakini hata kutoboa masikio kienyeji kwa mafundi ambao vifaa wanavyotumia havijatakaswa.

Lakini katika maeneo mengine mijini vifaa vya kusafishia kucha navyo huenda si salama inabidi kuwa makini hasa vile vinavyotumiwa kukwangua watu mbalimbali wanaojikusanya 'saloon' kwa wakati mmoja.

Kutoboa viungo vingine kama pua, macho na hata midomo kwa kutumia vifaa visivyotakaswa pia huleta virusi hivyo

Suala la ngono nalo linaelezwa kuwa ni chanzo na ushauri ni kila mmoja kulinda afya yake kwa kuachana na ngono zinazohatarisha maisha ukiwamo kuwa na wapenzi wengi na ulawiti.

Matumizi ya pombe kali na nyingine haramu kulewa kupindukia kunaharibu ini na kusababisha ugonjwa wa 'liver cirrhosis' unaoweza pia kusababisha virusi vya hepatisi kuingia kwenye ini.

**KUJIKINGA**

Kuachana na tabia zote hatarishi, kutambua watu wanaoweza kuambukizwa na kuwakinga, lakini pia kula vyakula vyenye lishe bora kunaweza kusaidia kulinda ini lisipate virusi hivyo, UN News inasema.

Chakula bora huongeza kinga ya mwili ili kuwa na afya bora ni vyema kula mlo kamili unaojaa matunda, mboga, vyakula vya nyuzinyuzi, visivyo vichafu (contermination) na kuachana na pombe, mafuta mengi, chumvi nyingi na hata sukari pia.

**DALILI**

Dalili za mwanzo hutokea ndani na miezi sita baada kuambukizwa virusi vya homa ya ini, hutokea kwa baadhi lakini si kila mtu.

UN News inasema mgonjwa mwenye maambukizi ya virusi vya homa ya ini hupoteza hamu ya kula, huwa na umanjano machoni, vinganja vya mikono, kucha au mwili mzima.

Lakini, ni vizuri kupima ili kujua iwapo una maambukizo ya homa ya ini ili wataalamu wakupe chanjo, ushauri na hata kuanza matibabu.

"Ili kujua kama umepata maambukizo ya homa y aini kitu muhimu ni kupima, vipimo ni rahisi na vinafanyika kwenye hospital mbalimbali, kwa hepatitis B kama mtu akipimwa na akagundulika kuwa hana maambukizo basi anaweza akapata chanjo ambayo itamkinga asiendelee kupata mambukizo," anasema Dk. Majinge.

**KUPIMA MUHIMU**

Homa ya ini ni tatizo la kiafya duniani linalohitaji kuzingatia kupima na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya katika hatua za kujikinga na ugonjwa huo unaoshambulia ini, lakini pia unaoambukizwa kwa kasi.

Tahadhari ni muhimu hasa wakati wa kumhudumia mgonjwa kuhakikisha kuwa unapomhudumia unatumia vifaa kinga kama glovu ili majimaji za mwili wa aliyeathirika zisiingize virusi mwilini mwaka.

Hata hivyo, kulala pamoja na mgonjwa hakuambukizi virusi hivyo.

## WANENAVYO MALENGA

### HEBU MSHUKURU MUNGU

Huku ulikupitia?
Mafiga uyapikia?
Sasa yamekunyokea?
Hebu mshukuru Mungu.

Korobo ikutumia,
Upate kumulikia,
Umeme wajivunia,
Hebu mshukuru Mungu.

Moshi ulilialia,
Kuni zikikuchulia,
Sasa gesi wapikia,
Hebu mshukuru Mungu.

Funza wali kupitia,
Vidole kujipindia,
Sasa mambo metulia,
Hebu mshukuru Mungu.

Shule kwenda wakimbia,
Pekua miguu pia,
Viatu unatilia,
Hebu mshukuru Mungu.

Watu unawasikia,
Et unadidimia,
Ugumu wakumbukia,
Hebu mshukuru Mungu.

Foleni kujipangia,
Sukari kununulia,
Sasa homu yakujia,
Hebu mshukuru Mungu.

Mungu amekujalia,
Umepata familia,
Maisha yametulia,
Hebu mshukuru Mungu.

Magumu ukipitia,
Zile hayajafikia,
Wa zidi jipigania,
Hebu shukuru Mungu.

Mlo unajipatia,
Nguo na malazi pia,
Na haja kupungukia,
Hebu mshukuru Mungu.

Kile unajitakia,
Uweze kukitumia,
Pesa ya kuamulia,
Hebu mshukuru Mungu.

Na wala hujafikia,
Vibaya ukafulia,
Riziki wajipatia,
Hebu mshukuru Mungu.

Mema uliyapitia,
Mabaya ya kuzidia,
Hujui ukoishia,
Hebu mshukuru Mungu.

Magonjwa ulipitia,
Wengi walishaishia,
Wewe watupumulia,
Hebu mshukuru Mungu.

Ajali wakumbukia,
Chupuchupu kutufia,
Kama walioishia,
Hebu mshukuru Mungu.

Donda linakuzidia,
Maumivu unalia,
Bado wajihudumia,
Hebu mshukuru Mungu.

Mfuko nimefulia,
Huduma wajipatia,
Bima ya kuhudumia,
Hebu mshukuru Mungu.

Wale walitangulia,
Ngazi mbele kupandia,
Sasa umewafikia,
Hebu mshukuru Mungu.

Ngazi ulizopandia,
Ndizo ulizoshukia,
Kwa amani watulia,
Hebu mshukuru Mungu.

Wengi tunawasikia,
Ngazi vema wapandia,
Pua wanaangukia,
Wewe mshukuru Mungu.

Au tunawasikia,
Juu wameshikilia,
Ngazi yawakatikia,
Wewe mshukuru Mungu.

Wengine wawasikia,
Kazi walalamikia,
Wewe kwako metulia,
Hebu mshukuru Mungu.

Vyeti unashikilia,
Kazi hujajipatia,
Bado watumainia,
Hebu mshukuru Mungu.

Neno linatuambia,
Yote yanatufikia,
Si ya kusikitikia,
Hebu mshukuru Mungu.

Hapo ulipofikia,
Wengine watamania,
Na hawatapafikia,
Hebu mshukuru Mungu.

Haya yatukumbushia,
Tusije sahaulia,
Tukabaki twatulia,
Bila mshukuru Mungu.

Yote yanayotukia,
Maisha tukisikia,
Muhimu kumwinamia,
Kwa maombi huyu Mungu.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com**
**0767223602**





# Wizi nyaya za umeme washamiri Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme nchini (TANESCO) Mkoa wa Dodoma, limebaini kuwapo kwa wimbi la wizi wa nyaya za umeme aina ya shaba hali inayorudisha nyuma jitihada za shirika.

Akizungumza jana na wananchi wa Kata ya Mnadani jijini hapo katika utoaji wa elimu kwenye maeneo yanayonufaika na miradi ya REA, Ofisa Usalama wa shirika hilo, Madega Dudu, alisema kuna tatizo la kuhujumu miundombinu ya umeme na watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Uhujumu.

Aliwataka wananchi kwenye maeneo yao kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele katika utoaji wa taarifa za wazi na siri kwa TANESCO ili hatua zichukuliwe mapema.

"Mpaka umeme huu unafikishwa hapa umesafiri kutoka mbali sana na umepita katika njia salama ndiyo maana unawaka, hivyo ni jukumu mojawapo la sisi Wanambwanga na Wanandachi kiujumla kulinda miundombinu iliyoko hapo na kuhakikisha usalama muda wote kwa kuwa shirika linaendelea na kubaini wahujumu na kuwachukulia hatua kama ambavyo sheria ya uhujumu inavyotaka," alisema.

"Kumekuwa na wizi wa nyaya za umeme aina ya shaba ambazo zinafungwa kwenye mashine umba (Transformer) ambazo zimewekwa kwa ajili ya ulinzi wa miundombinu ili kuepusha madhara, lakini kumekuwa na watu ambao wamekosea uzalendo wanakata na kuiba zile nyaya na kuturudisha nyuma, kwa hiyo ulinzi shirikishi ni muhimu kulinda hii miundombinu."

Kwa upande wake, Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja TANESCO mkoani humo, Sarah Libogoma, alisema shirika hilo linaendelea na uhamasishaji na utoaji elimu maeneo yanayonufaika na miradi ya REA na hadi kufikia mwisho wa awamu ya tatu ya miradi wananchi zaidi ya 30,000 wanatarajiwa kufikiwa na huduma.

Alisema kuwa miradi ya REA imelenga kufika maeneo yote ambayo umeme ulipita bila kusambazwa awamu zilizopita pamoja na kufikia maeneo ya pembezoni mwa jiji.

"Kata ya Mnadani ni iliyonufaika na miradi miwili ya REA ile ya ujazilizi na ya pembezoni, ambayo umeme umeshawashwa na tunategemea kuunganisha wateja zaidi ya 350 kwenye kata hii," alisema.

Alisema, pamoja na umeme kufika majumbani ni vyema wananchi walio eneo la mradi wakachangamka na kutumia fursa ya kukuza uchumi binafsi kwa kuomba huduma ya umeme mapema.

Naye Mwakilishi wa Mkandarasi wa mradi huo jijini Dodoma, Marlon Bulugu, alisema mradi kwa sasa upo ukingoni kazi inayoendelea ni kukamilisha uvutaji nyaya sehemu iliyobakia.

"Wiki ijao tunakamilisha kazi ya uvutaji nyaya kwa nguzo zilizobakia, tunachohitaji ni mwitikio wenu hivyo ni vyema wananchi mkaendelee na maombi ili nasi tuweze kukamilisha ufungaji mita mapema katika nyumba zenu," alisema.

Diwani wa Kata ya Mnadani, Paul Bakinye, aliishukuru TANESCO kwa kutoa elimu hiyo kwa wananchi.

TANESCO Dodoma inasimamia utekelezaji wa miradi miwili ya REA inayoendelea ndani ya jiji hilo ikiwamo wa ujazilizi unaotekelezwa na mkandarasi Derm Electrics na wa pembezoni (peri-urban) unaotekelezwa na mkandarasi Cylex Engineering.

## TAKUKURU yabaini ubadhirifu mapato watendaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani Dodoma, imebaini ubadhirifu wa mapato ya Sh. milioni 179.3 uliosababishwa na watendaji 17 kupitia mashine za kielektroniki za kukusanyia fedha (POS).

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapo, Sosthenes Kibwengo, alisema watendaji hao walichunguzwa na tayari mashauri 15 kuhusiana na ubadhirifu huo yamefikishwa mahakamani.

Alisema ufuatiliaji ulifanyika ili wahusika wapeleke fedha benki walizokusanya kupitia mashine za kielektroniki za kukusanyia fedha (POS) na kubaki nazo Sh. milioni 10.9 ziliokolewa.

Aliwataka wote wanaokusanya mapato ya halmashauri kuhakikisha wanayawasilisha benki kwa wakati na kuachana na matumizi ya fedha mbichi.

Kuhusu eneo la ukaguzi wa miradi, Kibwengo alisema kuna suala la kuchelewa kukamilika kwa miradi kinyume na mikataba jambo ambalo linapunguza ufanisi na kuongeza gharama.

Mkuu huyo alitoa wito kwa wananchi kutokomeza rushwa kwa kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo yao na kutoa taarifa kwa mamlaka hiyo wanapoona kuna rushwa au viashiria vya rushwa.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Athuman Ngenya, akizungumza na waandishi wa habari Idara ya Habari Maelezo jijini Dodoma jana, alipoelezea mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za shirika hilo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Serikali yashauriwa kudhibiti chakula cha ndani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Tanzania Fellowship of Churches (TFC), Dk. Godfrey Malasi, ameishauri serikali kudhibiti chakula kilichoko nchini kutoka nje ya mipaka ili kulifanya taifa kuwa na uhakika wa chakula.

Dk. Malasi, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye hafla ya kuwakabidhi vyeti vya kutambua mchango wa wadau mbalimbali waliofanikisha mkesha wa kitaifa wa maombi ya kuliombea taifa.

Alisema kutokana na uhaba wa mvua katika msimu wa kilimo uliopita kwenye maeneo mengi nchini mavuno yamekuwa kidogo hali inayotishia uhakika wa chakula.

"Ni lazima serikali kuanza kudhibiti chakula kilichoko nchini kwani hata Biblia inasema asiyetunza wa kwake ni mbaya kuliko mtu asiyeamini hivyo ni lazima kwanza kabla ya kuangalia watu wengine serikali itunze chakula kwa ajili ya watu wake kabla ya kupeleka nje," alisema.

Aidha, aliishauri serikali kuwa na maghala makubwa ya kuhifadhia chakula ambayo yatasaidia taifa kuwa na hifadhi ya chakula cha kutosha katika miaka mingi.

"Tunatumai kuwa pamoja na hofu zilizoko hapatakuwapo na njaa mwaka huu, lakini pia kila mtu anapaswa kuendelea kuliombea taifa ili kuondokana na changamoto mbalimbali," alisema.

Aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki sensa ya watu na makazi inayo tarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu.

Alisema moja kati ya eneo litakaloisaidia nchi kupiga hatua katika kutekeleza miradi yake ya maendeleo ni kupatikana kwa takwimu sahihi.

"Wito wangu kwa Watanzania kushiriki kikamilifu sensa ya watu na makazi ambayo itafanyika mwezi huu kwani itasaidia serikali kupata takwimu sahihi ambazo zitasadia kupanga bajeti kulingana na idadi halisi ya watu, naipongeza pia kwa namna ambavyo imejipanga naamini mwaka huu tutapata takwimu sahihi zaidi," alisema.

Kuhusu mkesha wa kuliombea taifa mwaka huu, Askofu alisema maandalizi yanaendelea na kuwataka wadau mbalimbali kuendelea kujitokeza ili kufanikisha tukio hilo kila mwaka.

"Mkesha huu wa kuliombea taifa kila mwisho wa mwaka tunaufanya ili kuombea amani pamoja na viongozi wetu kwani taifa bila amani haliwezi kusonga mbele hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kuchangia tukio hili," alisema.





Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti Tanzania (TARI), Dk. Geoffrey Mkamilo (kulia), akipata maelezo kutoka kwa watafiti wa Kituo cha Utafiti cha TARI Kibaha kilichoko mkoani Pwani kuhusu aina mpya ya mbegu ya mahindi wakati wa maonyesho ya wakulima na wafugaji yanayofanyika kitaifa katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Maonyesho Nanenane kubadilisha wakulima

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

WIZARA ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, imejipanga kuyatumia maonyesho ya wakulima na wafugaji maarufu Nanenane kubadilisha taswira ya wakulima kuanza kufanya kilimo chenye tija kwa kutumia teknolojia za kisasa ikiwamo mbegu bora.

Akizungumza na waandishi wa habari katika viwanja vya maonyesho ya wakulima vya John Mwakangale, mjini hapo, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema wamekuja na teknolojia zote mpya zilizogunduliwa na watafiti katika vituo vyake 17 vilivyoko nchini.

"Katika maonyesho yote ya wakulima Nanenane kuanzia ngazi ya kanda hadi yanayofanyika kitaifa hapa Mbeya, sisi kama TARI tumepeleka watafiti wa teknolojia zetu tulizogundua katika vitu vyetu vyote, lengo ni kumbadilisha mkulima kufanya kilimo cha kisasa na chenye tija," alisema Dk. Mkamilo.

Mkurugenzi huyo Mkuu wa TARI alisema, iwapo wakulima wanaofika katika maonesho ya wakulima na wafugaji yanayofanyika katika kanda mbalimbali watajitokeza kupata elimu ya teknolojia ya kisasa, ana uhakika tija katika kilimo itaongezeka na kukuza uchumi.

Alifafanua kuwa teknolojia hizo zilizoibuliwa na watafiti kutoka TARI pia zinaunganishwa katika mnyororo wa thamani katika mazao ya alizeti, mahindi, maharagwe, soya, chikichi na mpunga pamoja na mazao mengine.

Naye Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu wa TARI, Dk. Joseph Ndunguru, alisema teknolojia ya mbegu hizo zilizoibuliwa baada ya kufanyiwa utafiti zina uwezo mkubwa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchini.

Dk. Ndunguru alisema kutokana na teknolojia ya mbegu hizo, sasa vijana wanaweza kujikita katika kilimo kwa kufanya kilimo biashara kutokana na kuwa na uhakika wa kupata mazao na kuachana na kutegemea ajira za serikali.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha TARI Dakawa, kilichoko wilayani Mvomero, mkoani Morogoro, Dk. Jerome Mghase, alisema wamekuja na teknolojia mpya ya mbegu ya mpunga ambayo inamaliza changamoto kwa wakulima wanaolima katika maeneo yenye chumvi, magadi na wadudu waharibifu pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema aina hizo mpya za mbegu ya mpunga pia zimeonyesha kuongeza mavuno mengi pamoja na viinilishe muhimu kwa afya ya walaji na zimeshafanyiwa majaribio katika Ikolojia saba kwenye maeneo yanayolimwa mpunga nchini na kuleta tija kwa wakulima.

## TCB kuwapatia wakulima mbegu za kisasa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BODI ya Kahawa Tanzania (TCB), Nyanda za Juu Kusini wamejipanga kuwafundisha wakulima na kuwapatia mbegu bora na za kisasa za zao la kahawa ili kupata tija na faida.

Kauli hiyo iletolewa jana na Ofisa Ubora wa Bodi ya Kahawa Nyanda za Juu Kusini, Florian Ndunguru, alipozungumza na Nipashe kuhusu maandalizi ya bodi hiyo katika kuwasaidia wakulima kupitia maonyesho hayo ambayo kitaifa yanafanyika jijini Mbeya.

Ndunguru alisema kuwa maandalizi yote yamekamilika kwa ajili ya wakulima kwenda kujifunza mnyororo wa thamani wa zao la kahawa, kuanzia kupanda, kupalilia na kuvuna.

Alisema watayafikia makundi yote ya wakulima ambao wataonyesha nia ya kunufaika na zao hilo kwa kuhakikisha wanabadilika na kuachana na kilimo cha mazoea. Alisema Tanzania wanalima kahawa za aina mbili, aina Arabika na Robusta na Bodi ya Kahawa wanahakikisha aina hizo zinapatikana kwa wingi ili wakulima walime kwa wakati na kupata mavuno mengi.

Miongoni mwa wakulima akiwamo Saidiana Ngwisa, kutoka Kata ya Utengule, alisema kuwa Bodi ya Kahawa imekuwa ikiwapatia elimu sahihi ya namna bora ya kutunza kahawa shambani na baada ya kuvuna.

"TCB wamesaidia wakulima kulima kisasa ukilinganisha na ilivyokuwa awali tunalima kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo na kupata mavuno mengi ambayo yanasaidia kujikwamua kiuchumi na kumudu gharama za maisha," alisema.

Rashid Juma, mkulima wa Njelenje alisema wakulima wengi wamepata hamasa ya kulima zao hilo kutokana na elimu inayotolewa na wataalamu kutoka Bodi ya Kahawa Nyanda za Juu Kusini na maofisa ugani kutoka halmashauri mbalimbali za wilaya.

## Waendesha bodaboda watakiwa kuwa watangazaji wazuri miradi ya serikali

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAENDESHA bodaboda mkoani Mbeya wametakiwa kuwa mstari wa mbele kutangaza mazuri yote yanayofanywa na serikali ikiwamo miradi mbalimbali ya maendeleo kama ujenzi wa vituo vya afya, barabara, maji na uhamasishaji wa sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Rai hiyo imetolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, wakati akizungumza na madereva bodaboda wa Mkoa wa Mbeya, baada ya kukabidhi vifaa mbalimbali vya waendesha bodaboda.

Mfune alisema bodaboda ni kundi kubwa katika jamii na linapaswa kutumika kusaidia kwenye ulinzi na usalama pamoja na utoaji wa taarifa penye viashiria vya uhalifu pamoja na kusambaza jumbe zinazotolewa na serikali.

"Bodaboda ni kundi muhimu sana kwenye jamii yetu kwa sababu mnashirikiana na watu mbalimbali ambao naamini wanazo taarifa za kutosha, nawaomba mwendelee kushirikiana na serikali katika kufichua vitendo vya kihalifu, masuala ya maendeleo na mambo mengine ambayo yanalengo la kuijenga nchi," alisema Mfune.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodaboda Jiji la Mbeya, Aliko Fwanda alisema, wako bega kwa bega kuhakikisha miradi mbalimbali ya maendeleo inatekelezwa kwa ushirikiano na wananchi.



## Spika Tulia aunga mkono ujenzi wa shule za ghorofa

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Apson, amesema ujenzi wa shule za ghorofa utapunguza msongamano wa wanafunzi madarasani na kuipongeza Serikali ya Zanzibar kujenga shule hizo.

Dk. Tulia alisema hayo katika ziara yake ya kutembelea miradi ya sekta ya elimu katika majimbo ya uchaguzi ya Unguja na Pemba na kuangalia changamoto zinazowakabili wabunge katika majimbo yao.

Alisema elimu ndiyo kipaumbele cha serikali zote mbili katika kuona watoto wanapiga hatua kubwa ya maendeleo na kukabiliana na changamoto zilizoko ikiwamo kuingia katika ushindani wa soko la ajira.

Alisema ujenzi wa shule za ghorofa kwa kiasi kikubwa utapunguza msongamano wa sasa wa wanafunzi katika darasa moja na kuwapo kwa vipindi vitatu vya masomo katika siku moja.

Aidha, aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuzitumia vizuri fedha za ahuweni za UVIKO-19 katika sekta ya elimu kwa kujenga madarasa mapya hatua itakayowawezesha wanafunzi kujiamini.

Dk. Tulia aliwataka wabunge kuzitumia vizuri fedha za mfuko wa jimbo kwa ajili ya kutekeleza miradi inayowagusa wananchi katika sehemu zao.

Alisema madhumuni ya fedha za mfuko wa jimbo ni kwa ajili ya kuharakisha maendeleo pamoja na changamoto zinazoibuliwa na wananchi katika majimbo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, alisema wamepiga hatua kubwa katika kukabiliana na changamoto za sekta ya elimu kwa kujenga jumla ya madarasa 10,120 ambayo yamepunguza msongamano wa wanafunzi kusoma vipindi vitatu kwa siku.

Alisema kasi ya ujenzi wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Unguja pamoja na miradi ya ujenzi wa shule inayofanywa na wabunge na wawakilishi kwa kiasi kikubwa itapunguza msongamano wa wanafunzi kupata elimu.

# Abdullah: Saratani ina gharimu afya ya binadamu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema kuwa saratani ni moja ya magonjwa yasiyoambukiza na yenye kugharimu afya ya binadamu duniani.

Alisema kwa mujibu wa takwimu kutoka Wizara ya Afya Zanzibar ina wagonjwa wapya wa saratani wapatao 2,000 kila mwaka.

Aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya utoaji huduma kwa wagonjwa wa saratani, mjini hapo.

Alisema idadi hiyo kwa asilimia kubwa inatokana na utaratibu wa maisha ya watu wanayoishi hasa katika nchi maskini zinazoendelea.

"Watu wengi katika nchi hizi hawana mazoea ya kufanya mazoezi muda mwingi hutumika kukaa ofisini, darasani, kuangalia runinga na kutoshiriki katika mazoezi," alisema.

Alisema idadi hiyo inatokana na kula mlo ambao usio sahihi ikiwamo vyakula vyenye mafuta mengi, sukari na chumvi nyingi na ulaji wa vyakula vingi vya wanga, tofauti na mahitaji ya mwili.

Aliwataka wananchi kuendelea kuhamasishana kwa kubadilisha utaratibu wa maisha yao na kufanya mazoezi, kula mboga za majani, vyakula vyenye asili ya mizizi na nafaka ambazo hazijakobolewa na kula matunda badala ya kunywa juisi.

Alisema utaratibu huo utapunguza kiwango cha maradhi yasiyoambukiza Zanzibar ikiwamo saratani.

Aidha, alisema serikali inafanya maboresho ya sekta ya afya, kwa kujenga na kukarabati hospitali katika ngazi ya wilaya na mikoa na imetenga Sh. bilioni 36.67 kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba.

Kadhalika, alisema kuna mpango maalum wa kuzalisha wataalamu wa afya katika ngazi mbalimbali ili kuwa na madaktati wa kutosha ikiwamo bingwa wa saratani na kupunguza ukali wa athari za saratani.

Alisema uwapo wa majengo ni jambo moja, lakini vifaa tiba na madaktari ni jambo lingine na serikali imejipanga vizuri katika hilo na hatua za uajiri wa wataalamu wa afya tayari zinaendelea ili kuajiri madaktari na kuwahudumia wananchi.

Naye Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kwa mujibu wa takwimu za saratani duniani za mwaka 2018 (Glob can 2018), inakadiriwa zaidi ya watu 18,000,000,000, hupata saratani kila mwaka ikiongozwa na saratani ya mapafu, matiti, tumbo na tezi dume.

Alisema takribani watu milioni 9.6 hufariki kila mwaka duniani sawa na asilimia 21 ya vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukiza duniani.

Kwa upande wa Tanzania, alisema saratani inashika nafasi ya tano kwa wanaume na ya pili kwa wanawake kwa kusababisha madhara na vifo.

"Idadi ya wagonjwa wa saratani inaendelea kuongezeka nchini na duniani kwa ujumla. Ripoti ya mwaka 2018 ya Shirika la Umoja wa Mataifa la utafiti wa saratani inaonyesha kwamba takribani katika wagonjwa wapya 42,060, wagonjwa 28,610 hufariki kutokana na ugonjwa huu hapa nchini," alisema.

Vile vile, Zanzibar kuna wagonjwa wapya wapatao 12,000 kila mwaka kwa mujibu wa taarifa kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja na saratani za shingo ya kizazi, matiti, tezi dume, tumbo na saratani za damu zinaongoza.

Alisema serikali imejikita kutoa huduma za kinga na kuwafikia wasichana wenye umri wa miaka tisa hadi 14 zaidi ya asilimia 62 kuwapa chanjo ya HPV (Human Papilloma Virus) ili kuwakinga na saratani za shingo ya kizazi, pia kutoa chanjo ya homa ya ini (Hepatitis B) kwa watoto wote wanaozaliwa. Serikali pia inatibu watu waliopata maambukizi ya homa ya ini C (Hepatitis C) ambayo itawakinga na saratani ya ini.

Alisema kwa sasa serikali imeanza mchakato wa kuanzisha huduma za mionzi tiba (radiotherapy), kuipunguzia mzigo Hospitali ya ORCI na kuwarahisishia wananchi wake kupata huduma hiyo.

Mazrui alisema changamoto inayo wakabili wagonjwa wa saratani pamoja na familia zao, vipimo, maumivu makali na maisha ya mateso anayoishi mgonjwa wa saratani hasa kwa wale ambao wamegundulika na ugonjwa ukiwa kwenye hatua kubwa.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa na mkewe Mama Mariam Mwinyi wakati akimpongeza mwanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari ya Fidel Castro Pemba, Kassim Khamis Omar kwa kufaulu vizuri mtihani wake wa Taifa wa kidato cha sita mwaka huu, katika hafla ya chakula maalum, pia alitoa zawadi kwa wanafunzi waliofaulu vizuri mitihani yao, hafla iliyofanyika viwanja vya Ikulu ndogo Pagali Pemba mwishoni mwa wiki. **PICHA: IKULU**

# Kamishna Hamad aahidi ushirikiano mapambano udhalilishaji kijinsia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, amesema yupo tayari kushirikiana na wanaharakati wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ili vitendo hivyo vidhibitiwe na kuongeza kasi ya upelelezi na watuhumiwa kufikishwa mahakamani haraka.

Kamishna huyo aliyepata uteuzi hivi karibu aliyasema hayo makao makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar, wakati alipofanya mazungumzo na wanaharakati wa kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo asasi za kiraia.

Alisema Jeshi la Polisi limejipanga kutokomeza vitendo hivyo ikiwamo kutoa elimu na kufanya mazungumzo na mikutano mara kwa mara na wanaharakati.

Alisema miongoni mwa vikwazo katika kutokomeza vitendo hivyo ni jamii kushindwa kutoa ushirikiano ikiwamo kutoa ushahidi wa kesi hizo mahakamani.

Alisema zipo kesi zinalazimika kufutwa mahakamani kwa sababu wahusika hawapo tayari kutoa ushahidi ambao ni miongoni mwa sehemu muhimu ya kuwatia hatiani watuhumiwa.

Mkurugenzi Mkuu wa kijiji cha kulea watoto yatima (SOS), Asha Salim Ali, aliliomba Jeshi la Polisi kuongeza ushirikiano utakaosaidia kuyafikia malengo yake ikiwamo kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na waathirika wake wakubwa ni wanawake na watoto.

Alisema bado jamii haijaelimika zaidi kupambana na udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo baadhi ya wazazi kutotoa ushirikiano wakati wanapotakiwa kufuatilia kesi za udhalilishaji mahakamani na vituo vya polisi.

Aidha, aliliomba Jeshi la Polisi kuacha kusuluhisha kesi za udhalilishaji katika vituo vya polisi kwa sababu zipo taarifa kwamba baadhi ya wananchi wanaowasilisha malalamiko yao hupewa ushauri wa kusuluhisha kesi hizo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 616 OF 2022 in the matter of the estate of the late PAULINA SIRIRI MAYUGA and in the matter of application for letters of administration by ROBERT SIMON BARUTI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration)is made to the to the above-named petitioner.

Objections to the grants should be filed on or before the 13 day Of 09,2022

**Dated at dar es salaam this 15 day of 07,2022**

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KAHAMA**
**WILAYA YA KAHAMA**

**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA 40 YA 2022**
**DAUDI NZINGULA.........MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**JUMA SAYI.............MJIBU RUFAA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: JUMA SAYI**

**POPOTE ALIPO.**

Kwa kuwa Muomba rufaa ameleta Rufaa ya Madai, hapa Mahakama ya Wilaya katika Shauri tajwa hapo juu, ambalo litasikilizwa terehe 10/08/2022.
Unaamuriwa kuhudhuria Mbele ya Mahakama hii mnamo tarehe 10/08/2022, saa 2:30 asubuhi bila kukosa au kuchelewa, ambapo siku hiyo ni siku ya kusikilizwa kwa Shauri hilo, hivyo unapaswa kuleta utetezi wako au pingamizi la Maombi haya.
Fahamu kuwa usipohudhuria siku hiyo, Shauri linaweza kuendelea kusikilizwa na kutolewa hukumu upande mmoja bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Mahakama hii leo terehe 18 Mwezi Julai Mwaka 2022.

.............................................
**Donasian J.A**
**HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA KAHAMA.**

---

**KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA UPENDO MAKUNDI P.O BOX 1229 DODOMA TUTAFANYA MNADA WA HADHARA TAREHE 31/08/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA KIWANJA NO. 71 KITALU "D" ILAZO NORTH, MALI YA PASTORY PATRICK MPONDA BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO. MNADA UTAFANYIKA MAHALI AMBAPO KIWANJA KIPO

**KWA MAWASILIANO PIGA NO. 0688729841/ 0657222838.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No.105 of 2022**
**In the matter of the Estate of the late of the late**
**CELESTINA CASMIRY JOHN**
**of Changombe within Dodoma City.**
**AND**
**In the matter of application for letters of administration by**
**EVA AUGUSTIN MWENDA.**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 16 Day of 08, 2022
**Dated at Dodoma this 26 day of 07,2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---

# KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN ALEX TALALIKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina **ZACHARIA MICHAEL MAGILE** namba za usajili **T848CCK** aina ya **TOYOTA IST** Rangi Nyeupe. Chassis **No. NCP600114663.** **Engine No. 2NZ-FE-1298** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/48244/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya MOSHI**
**Kituo cha MWIKA mkoa KILIMANJARO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 29/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU KINYAUO HOSEA ABEL wa MWIKA/BERLINE UJERUMANI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA EMIL ABEL MALLE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Imetolewa leo Tarehe 21 Mwezi 07 Mwaka 2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**
**Shauri la Madai Na. 123/2022**
**Jina la Mdai: KIKUNDI CHA EFATA**
**Jina la Mdaiwa: DEVOTHA MAKALANGA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: DEVOTA MAKALANGA**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ya **MADAI YA FEDHA SHILINGI MILIONI NNE TU (Tsh. 4,000,000/-)** Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **05 Mwezi 08 Mwaka 2022 saa 2:00 asubuhi.** Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 Mwezi 07 Mwaka 2022.**

.............................................
**HAKIMU**

---

**TEGEMEZA AUCTION MART LIMITED**
**P.O.BOX 77593**
**MBEZI BEACH, DSM**

Kwa mamlaka ya mahakama kuu kitengo cha kazi pamoja na mahakama ya mwanzo kigamboni tunawajulisha mnamo Tarehe 18/8/2022 kutakuwa na mnada wa hadhara uuzaji wa vitu tajwa hapo chini:

| AINA YAMALI | MAHALI PA MNADA | MADAI |
|---|---|---|
| Gari aina ya IST namba T626 DQK | Mbezi beach bondeni<br>Muda: saa 4: 00 asubuhi | Mdaiwa : Malmo Development LTD. Mdai:<br>The Labour Commissioner<br>Kesi namba: 455/2020 |
| Pikipiki aina ya TVS MC 101 BPV | Mbezi beach , bondeni | Mdaiwa: Idrisa Rajabu<br>Mdai: Maria Thadeo |

**Masharti ya mnada**
Unatakiwa kulipa asilimia 25% siku ya mnada baada ya siku 14 unamalizia.
Mali inauzwa kama ilivyo .
Gharama za kubadili umiliki ni za mteja .

**Kwa mawasiliano zaidi 0719-187677.**

---

# KUPOTEA KWA VYETI



**NICKAS R. VENANCE** anatangaza kupotea kwa vyeti; cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4087-0044** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **WIZA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013 ,** cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0142-0596** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **GALANOS SECONDARY SCHOOL** mwaka **2016** na Cheti cha chuo chenye usajili namba **14302002/T.16** kilichotolewa na **MZUMBE UNIVERSITY** mwaka 2019 . kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TARIFA : GBA/K/B.1/1/334**

---

# KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOHN DESIDELIUS KIHWILI WA KITUMBAROMO – MBINGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye Namba za usajili **MC 652 DJE** aina ya **HAUJUE** kwa Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
**Taarifa ya Polisi : RUV/MBI/RB 280880/2022.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 16/2021.**

**SHEMI SAID SHAWEJI————————MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**1.BATIAN MATEI**
**2.THEODOSIA LUOGA**
**3.NYAMAKO AUCTION MART &COURT BROKER —-WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**
Mjibu maombi namba tatu anataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako.Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 11/08/2022 saa 2.00 asubuhi.Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zenu za utetezi.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.
**Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 29/07/2022.**

——————————————————
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) SONGEA.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA NZEGA**
**MAOMBI YA ARDHI NA.12 YA MWAKA 2022**
- **MASOLWA SALAMBA**
- **CHARLES MWAIPONYA......... MUOMBAJI**

**DHIDI YA**
- **ELIAS KUSHOKA**
- **MWANDU MWAIPONYA**
- **CHRISTOFA KUSHOKA**
- **MAYUNGA JOHN.........WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi **BW. MWANDU MWAIPONYA** popote ulipo unafahamishwa kwamba **BW. ELIAS KUSHOKA** na **CHARLES MWAIPONYA** wamefungua maombi ya Ardhi **Na. 12/2022** katika baraza la Ardhi na nyumba la wilaya lililopo Nzega. Shauri husika linapanga kutajwa tarehe **24/08/2022** saa **2:30** asubuhi. Hivyo unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku **14** kuanzia tarehe ya kutolewa tangazo hili. Vielelzo vyote vya kesi vinapatikana katika masjala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba (W)- Nzega.
Ufahamu kwamba usipohudhuria maombi husika yatasikilizwa bila ya wewe kuwepo/kutoa utetezi wako na kutolewa hukumu.
**Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 27/07/20222.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......16/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: KHADIJA MRISHO MUYA WA MAZIMBU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA FATUMA SELEMANI MAGOGA**

**TANGAZO**
(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 25 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 01 mwezi 08 mwaka 2022**

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA WAGING'OMBE**
**KITUO CHA WAGING'OMBE MKOA WA NJOMBE**
**Usimamizi wa Mirathi Na......08/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: SIMIONI KIPALILE WA ITENGELO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JOSEPH ALIMASI KIPALILE**

**TANGAZO**
(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 26 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 07 mwaka 2022**

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Rais Biden akutwa tena na UVIKO-19

**WASHINGTON,** MAREKANI

DAKTARI binafsi wa Rais wa Marekani, Joe Biden, Dk. Kevin O Connor amesema rais huyo amekutwa tena na virusi vya UVIKO-19 licha ya kutoonyesha dalili yoyote kuwa anaugua ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA Kiongozi huyo alifanyiwa vipimo Jumamosi baada ya kupona kutokana na maambukizi ya wiki iliyopita, na kwamba huenda atakaa karantini katika ikulu ya White House baada ya maambukizi hayo mapya kugundulika.

Dk. O Connor alisema kwamba Rais Biden ana dhamira ya kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa karibu naye wanalindwa dhidi ya maambukizi.

Aliongeza kwamba Rais Biden alikuwa amepona kutokana na maambukizi ya awali, lakini yamerudi tena, suala analosema hujitokeza kwa asilimia ndogo ya wagonjwa wanaotumia dawa aina ya Paxlovid kutibu maambukizi ya awali.

Mshauri mkuu wa kiafya wa Rais alisema hali ya kupatikana kuwa na virusi baada ya kupata chanjo haina historia ya kuwa na hatari yoyote.

Pia alibainisha kuwa Biden ataendelea kufanya kazi kwenye ofisi yake wakati leo 'jana' akilazimika kuahirisha ziara iliyokuwa impeleke kwenye jimbo lake la Delaware. **VOA**

# Wananchi Senegal wapiga kura kuwachagua wabunge

**DAKAR,** SENEGAL

WANANCHI nchini Senegal wamepiga kura katika uchaguzi wa wabunge huku upinzani ukiwa na matumaini ya kulazimisha ushirika na Rais Macky Sall katika kuunda serikali na kuzuia nia yake ya kuwania muhula wa tatu.

Sall ambaye alichaguliwa mwaka 2012 kwa muhula wa miaka saba na kuchaguliwa tena mwaka 2019 kwa muhula wa miaka mingine mitano, alishutumiwa kwa kutaka kuvunja sheria kuhusu kikomo cha mihula miwili na kugombea tena mwaka 2024.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA, bado kiongozi huyo hajasema wazi msimamo wake juu ya suala hilo, huku ikielezwa kuwa kushindwa kwa wafuasi wake katika uchaguzi uliofanyika Jumapili kunaweza kuvuruga mipango yake.

Chanzo cha kuaminika kilicho karibu na wizara ya mambo ya ndani kinachohusika na uchaguzi kiliiambia AFP, kuwa hadi kufikia mchana, idadi ya waliojitokeza kupiga kura ilikuwa asilimia 22, na kwamba matokeo ya kura yanatarajiwa kabla ya Ijumaa ya wiki hii.

Aidha, inadaiwa kuwa idadi ya waliojitokeza kupiga kura katika vituo kadhaa vya kupigia kura ilionekana kuwa ndogo.

**VOA**

# Kikwete ateuliwa kuwa kiongozi timu uangalizi uchaguzi Kenya

**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa Awamu ya Nne wa Tanzania, Dk. Jakaya Kikwete, ameteuliwa kuongoza ujumbe wa wachunguzi wa uchaguzi mkuu wa nchini Kenya kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Kenya inatarajia kufanya uchaguzi mkuu Agosti 9, mwaka huu, na joto la kisiasa likiendelea kuongezeka huku wagombea nafasi ya urais, ubunge na ugavana wakizunguka nchi nzima kujinadi na kumwaga sera zao.

Ujumbe huo wa maofisa 52 utakuwa ukisimamia na kuangalia kiwango cha matayarisho na utekelezaji mzima wa uchaguzi mkuu wa Kenya unaotarajiwa kufanyika Agosti 9, mwaka huu.

Aidha, Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, akizungumza katika mkutano alioufanya na wananchi jana, alimtaka Naibu Rais ambaye ni mmoja wa wapinzani wake anayegombea urais William Ruto kuacha siasa za kutukanana na kuwaambia watu kuwa ana mpango wa kumuua.

Alisema katika suala linaloendelea nchini humo hakuna haya ya kurushiana matusi huku akisisitiza Wakenya kufanya kile ambacho ni sahihi na stahiki.

"Hakuna haja ya matusi jamani, wala kuingilia watu, kila mtu nikiwamo mimi ana uhuru wa kupigia debe yeyote ambaye anamtaka, kwa hiyo uamuzi utakuwa wa wananchi," alisema na kuongeza;

"Nikikujibu kwa sababu umesema mambo ya uongo hakuna haja ya kuwaambia watu nataka kukuua, si mmenitusi karibia miaka mitatu, kuna mtu amewagusa, hiyo miaka mitatu si nimekuwa kwenye kiti si nilikuwa na uwezo, nikiwa sina uwezo ndio niko na time (muda) ya kukutafuta," alisema Kenyatta.

"Uza sera zako, achana na mimi, nafanya kazi yangu nimalize, nyinyi kaombeni kura wananchi wakiwapatia sawa, wakiwanyima twende nyumbani pamoja shida iko wapi, si dunia itaendelea," alisema Kenyatta.

Aidha, hivi karibuni Rutto alimwomba Kenyatta msamaha walipotofautiana baada ya kukamilika kwa uchaguzi wa 2018.




Rais mstaafu wa Tanzania ambaye ni Kiongozi wa Timu ya Waangalizi wa Uchaguzi Mkuu wa Kenya, Jakaya Kikwete, akihutubia nchini Kenya jana. **PICHA: EAC**

# Maelfu ya watoto wakosa makazi DRC

**KONGO,** DRC

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF) limesema maelfu ya watoto wameyakimbia makazi yao mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ambako jeshi la taifa linapambana na waasi wa M23.

Taarifa mpya ya shirika hilo ilieleza kuwa tangu mwezi Machi mwaka huu, watu zaidi ya 190,000 walilazimika kuondoka katika vijiji vyao wilaya za Rutshuru na Nyiragongo, ikibainisha kuwa nusu ya idadi hiyo ni watoto.

Mkurugenzi Mkazi wa UNICEF huko DRC Grant Leaity, baada ya kufanya ziara katika wilaya ya Rutshuru juma lililopita, alisema maelfu ya watoto wanakabiliwa na vitisho na hawawezi kupata huduma za msingi ambazo ni muhimu kuwanusuru katika mzozo huo.

"Watoto wataendelea kukabiliwa na masaibu hayo, kwa sababu bado watu wana hofu kurejea katika vijiji vyao," alisema Leaity.

Ofisa huyo wa Umoja wa Mataifa pia alikutana na watu hao walioyakimbia makazi yao, walioko katika eneo la Kalengera, ambako wakimbizi wa ndani wanawazidi mara mbili wenyeji.

"Familia za wakimbizi wa ndani zinahitaji msaada wa dharura wa chakula, vifaa vya nyumbani, huduma za afya na maji safi, pamoja na vifaa vya usafi," ilisema UNICEF katika taarifa yake.

Aidha, shirika hilo la msaada kwa watoto limeongeza kuwa wakati mahitaji ya msaada huo yakiongezeka kwa kasi, upatikanaji wake unawasili kwa kusua sua.

Pia taarifa ilisema kutokana na ukosefu wa msaada, baadhi ya watu wanalazimika kurudi katika vijiji vyao, katika maeneo ya mstari wa mbele wa mapigano ambayo sio salama, huku ikiongeza kuwa jumuiya ya kimataifa haina budi kuchukua hatua za haraka ili kuepusha madhila zaidi kwa watoto wanaokumbwa na utapiamlo na kupindukia.

Vile vile ilibainisha kuwa Wilaya ya Rutshuru imejikuta katika hali tete miezi ya karibuni, kutokana na uwepo wa waasi wa M23 ambao wamekuwa wakipigana na jeshi la serikali ya Kongo.

M23 ni vuguvugu linalodhibitiwa na wapiganaji kutoka jamii ya Watutsi ambalo lilisambaratishwa mwaka 2013, lakini lilichukua tena silaha mwaka 2021 na kuanzisha mashambulizi mapya dhidi ya jeshi la serikali na ujumbe wa Umoja wa Mataifa wa kulinda amani (MONUSCO) na limeweza kuyakamata na kuyashikilia maeneo kadhaa.

Serikali ya Kinshasa inaituhumu Kigali kuwaunga mkono waasi hao, tuhuma ambazo Rwanda imezikanusha.

**DW**

# Watu 19 wafariki dunia mafuriko Marekani

**APPALACHIA,** MAREKANI

WATU 19 wameripotiwa kufariki kutokana na mafuriko yaliosababishwa na mvua kubwa katika eneo la Appalachia kaskazini mwa jimbo la Kentucky nchini Marekani huku likitajwa kuwa janga kuwa zaidi kuwahi kulikumba eneo hilo.

Gavana wa Jimbo la Kentucky, Andy Beshear, alisema kuwa huenda idadi ya waliofariki ikaendelea kuongezeka, akibainisha kwamba mamia ya makazi ya raia na maeneo ya biashara yamejaa maji.

Rais wa Marekani, Joe Biden, ametaja mafuriko hayo kama janga kubwa ambapo ameamuru usaidizi wa haraka kwa walioathiriwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na RFI miongoni mwa waliofariki ni pamoja na watoto sita akiwamo mtoto wa mwaka moja. Aidha, wanasayansi walieleza kuwa mabadiliko ya tabia nchi yamechangia kutokea kwa matukio kama hayo ya mafuriko ya Kentucky.

Ilibainisha kuwa takribani watu 33,000 katika eneo hilo wanakabiliwa na tishio la umaskini, umeme kukatika kutokana na mafuriko hayo, barabara kutopitika baada ya kuzibwa na maporomoko ya udongo.

Vile vile japokuwa eneo husika limekuwa likikumbwa na matukio ya mafuriko, mamlaka katika mji huo zimethibitisha kuwa hayajawahi fikia kiwango cha hivi sasa.

Pia kutokana na janga hilo watu wametakiwa kuhamia katika maeneo salama wakati huu mvua ikitarajiwa kuendelea kunyesha. **RFI**



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kushoto) akiwa pamoja na wakurugenzi wa taasisi washirika wa CRDB Bank Marathon, wakati wa kutambulisha vifaa vitakavyotumika katika msimu wa tatu wa mbio hizo zitakazofanyika Agosti 14, mwaka huu. Wengine kutoka kulia ni Prof. Mohamed Janabi, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Brenda Msangi, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya CCBRT, Julius Magabe, Mkurugenzi Mtendaji wa Sanlam, Mkurugenzi Mtendaji wa Cocacola Kwanza, Unguu Sula, Mkurugenzi wa Maendeleo na Biashara, Mkurugenzi wa Masoko Johari Rotana, Brigitte Alfred na Mkuu wa Kitengo cha Fedha Alliance, Ahamad Luoga katika hafla iliyofanyika Hoteli ya Johari Rotana, Benki ya CRDB pia ilitangaza jumla ya zawadi za shilingi milioni 100. **MPIGAPICHA WETU**

# MILIONI 100 KUSHINDANIWA MBIO ZA BENKI YA CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku 12 kuelekea msimu wa tatu wa mbio za Benki ya CRDB (yaani CRDB Bank Marathon), zitakazofanyika Agosti 14, mwaka huu, Sh. milioni 100 zitashindaniwa katika mbio hizo zinazotarajiwa kushirikisha wakimbiaji zaidi ya 6,000.

Hayo yalibainishwa jana na uongozi wa benki hiyo wakati wa hafla fupi iliyokutanisha wadau na washirika wa CRDB Bank Marathon kwenye Hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema katika mbio za mwaka huu, benki hiyo imefanya maboresho makubwa kwenye zawadi ili kuongeza ushindani miongoni mwa washiriki, lakini kuendana na hadhi ya kimataifa ambayo mbio hizo zilipata mwaka jana.

"Katika mbio ndefu za Km 42.2, washindi wa kwanza kwa upande wa wanaume na wanawake watapata Sh. milioni 10 kila mmoja. Washindi hawa pia watapata zawaidi ya kulala usiku mmoja hapa Johari Rotana pamoja na vocha za zawadi katika duka la Justfit," alisema.

Akitoa majumuisho ya zawadi hizo, Mkurugenzi wa Mawasiliano Benki ya CRDB, Tully Mwambapa, alisema katika mbio hizo zikiwamo za Km 21.1, Km 10, kilometa tano na baiskeli Km 65, washindi sita wa kwanza watapewa zawadi za fedha taslimu.

Tully aliongeza kuwa pia kutakuwa na zawadi kwa makundi maalum ya wazee, watoto na wakimbiaji waliovaa kipekee. "Jumla ya zawadi hizi zote zitakazotolewa kwa washindi ni Sh. milioni 100," alisema Tully.

Katika hafla hiyo, Benki ya CRDB pia ilitambulisha vifaa vitakavyotumika katika msimu wa tatu wa CRDB Bank Marathon ikiwamo medali, fulana, kofia na mfuko wa kuwekea vifaa (back-pack) ambazo washiriki wa mbio hizo watapewa.

Kwa upande wa usajili, Nsekela alisema mpaka jana, tayari watu zaidi ya 4,200 walikuwa wameshajisajili kushiriki mbio hizo.

Nsekela alibainisha kuwa kati yao, 801 ni wakimbiaji kutoka nje ya nchi na kutoa rai kwa Watanzania kuchangamkia nafasi zilizobaki.

"Niwashukuru wale wote waliojisajili katika mbio hizi. Kwa wale ambao bado, niwasihi kutembelea tovuti yetu ya "http://www.crdbbankmarathon.co.tz" kujisajili, mtu binafsi atachangia Sh. 40,000 na washiriki kupitia vikundi ni Sh. 30,000," alisema.

Aliongeza: "Katika siku hizi chache zilizobaki tungependa zaidi kuona Watanzania wengi wakijitokeza kujisajili na kushiriki kwa wingi kwani hii ni marathon yetu na tungependa pia kuona zawadi hizi zikibaki nyumbani."

Nsekela alitumia fursa hiyo kumshukuru Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika mbio hizo.

Alisema viongozi mbalimbali tayari wameshajisajili kushiriki wakiwamo Waziri wa Michezo, Sanaa na Utamaduni, Mohamed Mchengerwa.

Viongozi wengine waliojisajili kushiriki ni pamoja na Naibu Waziri wa Michezo, Pauline Gekul, Naibu Spika, Mussa Zungu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Innocent Bashungwa, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, na Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo.

Akizungumza kwa niaba ya washirika wa CRDB Bank Marathon, Mkurugenzi wa Mkuu wa Sanlam, Julius Magabe, alisema kampuni yao inajivunia kuwa washirika wa CRDB Bank Marathon kutokana na mbio hizo kujikita zaidi katika kuhamasisha watu kusaidia jamii.

"Tunaishukuru Benki ya CRDB kwa kuandaa mbio hizi zinazowaleta Watanzania kushiriki ili kutatua kero katika jamii. Sanlam ni kampuni ambayo inajali afya na mazingira ya watu wake, hivyo tuna kila sababu ya kushiriki katika mbio hizi," alisema Magabe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, aliishukuru Benki ya CRDB kwa kuandaa mbio hizo ambazo zinalenga kukusanya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kusaidia gharama za matibabu kwa kinamama wenye ujauzito hatarishi katika Hospitali ya CCBRT na upasuaji kwa watoto wenye matatizo ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

## Kocha Polisi TZ akunwa viwango

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Polisi Tanzania, Joslin Bipfubusa, amesema ameridhishwa na kiwango kinachoonyeshwa na wachezaji wake wakati huu wakijiandaa na msimu mpya unaotarajiwa kuanza baadaye mwezi huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kocha huyo amesema wachezaji ambao amewakuta, wanastahili kuendelea nao kutokana na uwezo wanaouonyesha kwa sasa.

"Wachezaji wanaonyesha uwezo mzuri, ninaamini kitakuwa kikosi ambacho kitaleta ushindani kwenye msimu ujao," alisema Bipfubusa.

Kocha huyo alisema kikubwa anachokifanya kwa sasa ni kuwapa mazoezi ya utimamu wa mwili ili kuwaweka kwanza sawa.

"Ninahitaji michezo mingi ya kirafiki kabla hatujaingia kwenye msimu mpya," alisema kocha huyo.

## Kundemba kusajili 10 na kufyeka tisa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KUELEKEA msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar utakaoanza baadaye mwezi huu, timu ya Kundemba FC, inatarajia kusajili wachezaji wapya 10.

Kundemba itacheza Ligi Kuu ya Zanzibar msimu huu baada ya Kupanda daraja msimu uliomalizika wa 2021/22.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nadir Kijo, alisema timu hiyo itasajili wachezaji hao kutoka madaraja tofauti ya Zanzibar ili kukiongezea nguvu kikosi chake.

Alisema timu hiyo inatamani kusajili nyota kutoka nje, lakini kutokana na ukata itaendelea kusajili wachezaji ndani ya Zanzibar na pengine ikasajili mchezaji mmoja au wawili kutoka nje ya Zanzibar.

"Unajua timu nyingi hizi za uraiani changamoto kubwa ni fedha, hususan katika kipindi hiki cha usajili timu inatamani kusajili wachezaji wazuri ambao wanaweza kukupa matokeo mazuri, lakini changamoto inakuja kwenye fedha ila tutajitahidi kusajili wachezaji wazuri kutoka hapa Zanzibar," alisema.

Mbali na kusajili wapya 10, kocha huyo alisema pia wanampango wa kuwaacha wachezaji wake tisa ambao viwango vyao haviwezi kuhimili mikikimikiki ya Ligi Kuu Zanzibar.

## ZISIKUPITE

### DE JONG NA CHELSEA
CHELSEA wanatoa ofa kwa Barcelona ili kumsajili Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25. ***(Sport)***

### WERNER APEWA OFA
KLABU ya Chelsea imeiomba Klabu ya Real Madrid kumsajili mshambuliaji wake, Timo Werner ambaye hana nafasi kwenye kikosi hicho cha Blues kwa sasa. ***(Marca)***

### FOFANA, DUMFRIES WAWINDWA
CHELSEA inajaribu kutaka kumsajili mlinzi wa kati wa Ufaransa, Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 21 kutoka Leicester City na mlinzi wa Uholanzi, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 26 kutoka Inter Milan. ***(Athletic)***

### BARNES ATAKIWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United inamfuatilia winga wa Leicester City na England, Harvey Barnes, baada ya kukataliwa kumsajili James Maddison mwenye umri wa miaka 25. ***(Mail)***

### VAN DIJK NA SALAH
MLINZI wa Uholanzi, Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 31, amesema mchezaji mwenzake wa Liverpool, Mohamed Salah (30), pengine aliathirika na mazungumzo ya mkataba mpya msimu uliopita, lakini fowadi huyo wa Misri hivi sasa anacheza "akiwa huru na amani" baada ya kusaini mkataba mpya. ***(Liverpool Echo)***

### GUEYE AKARIBIA EVERTON
KLABU ya Everton inaendelea na mazungumzo na Paris St-Germain wakiwa wanakaribia kumsajili kiungo wa Senegal, Idrissa Gueye mwenye umri wa miaka 32 pale Goodison Park. ***(Times)***

### KALAJDZIC AWANIWA
KLABU ya Manchester United inaangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Stuttgart, Sasa Kalajdzic mwenye umri wa miaka 25. ***(Mail)***

### ANGELINO AMULIKWA BARCA
MLINZI wa kushoto wa RB Leipzig, Angelino mwenye umri wa miaka 25, analengwa na Barcelona kama wakishindwa kumsajili, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 31 kutoka Chelsea. ***(Sport)***

### BAYERN HAISAJILI
OFISA Mtendaji Mkuu wa Bayern Munich, Oliver Kahn, ambaye alisema straika wa Tottenham na England, Harry Kane ni "ndoto yetu ya baadaye", amesema klabu hiyo ya Ujerumani haina mpango wa kumsajili mshambuliaji kwa sasa. ***(90 Min)***

### BELOTTI ATAKIWA ROMA
AS Roma imetoa ofa ya kutaka kumsajili straika wa Italia, Andrea Belotti mwenye umri wa miaka 28, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kuondoka Torino kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Football Italia)***

### TAVERNIER BASI TENA
KOCHA wa Bournemouth, Scott Parker amesema dili la kumsajili kiungo wa Middlesbrough, Marcus Tavernier mwenye umri wa miaka 23, kwa sasa limefungwa. ***(Teesside Live)***

### FIRMINO AKATAA JUVE
FOWADI wa Liverpool, Roberto Firmino amehusishwa na kuwaniwa Juventus, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amesema hataki kuondoka hapo Anfield. ***(Liverpool Echo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# XAVI: SIJUI KAMA DE JONG ATABAKI BARCA

**Rais wa klabu, Joan Laporta amekuwa akisema atafanya kila awezalo kumbakisha Camp Nou, lakini...**

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi amefichua kuwa hajui kama Frenkie de Jong bado atakuwa kwenye klabu hiyo ifikapo mwishoni mwa dirisha la usajili huu wa majira ya joto.

Kwa mujibu wa 90min, Manchester United wamekubali ada ya euro milioni 85 kwa ajili ya kumsajili kiungo huyo, lakini dili hilo linasitishwa kutokana na msisitizo wa Mholanzi huyo kulipwa karibu euro milioni 20 ikiwa ni malimbikizo ya mshahara wake.

Rais wa Barca, Joan Laporta amekuwa akisema mara kwa mara atafanya kila awezalo kumbakisha De Jong hapo Camp Nou, ingawa amekiri hili huenda lisiwezekane.

Na Xavi amethibitisha kuwa bado kuna mashaka iwapo De Jong atasalia Katalunya msimu ujao, ingawa wazo lake la kumchezesha kama beki wa kati halikusudiwi kuchukuliwa kama ishara kwamba hayumo katika mipango ya klabu hiyo.

"Sijui kama (De Jong) atasalia hapa. Bado kuna wakati na mambo mengi bado yanaweza kutokea," alisema Xavi baada ya ushindi wa mabao 2-0 wa Barcelona dhidi ya New York Red Bulls, juzi.

"Kwa sasa yeye ni sehemu ya timu, kama kila mtu mwingine. Kucheza kama beki wa kati katika michezo mingine haikuwa ishara kwamba anaondoka.

"Sihitaji kutuma ishara uwanjani. Ninaweza kuzungumza moja kwa moja na wachezaji wangu."

Wakati De Jong anataka kupokea mishahara yake ambayo haijalipwa, Barcelona imekuwa na shughuli nyingi ya kutumia fedha msimu huu.

Franck Kessie na Andreas Christensen wamejiunga kwa uhamisho wa bure, wakati Raphinha, Robert Lewandowski na Jules Kounde wamesajiliwa kwa ada kubwa.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,019,3

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 03 AGOSTI 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/08/22 | 20:00 | Landskrona Bois vs Skovde Aik | 2.28 | 3.47 | 3.01 |
| 02. 03/08/22 | 20:00 | Dalkurd FF vs Norrby IF | 2.96 | 3.57 | 2.26 |
| 03. 03/08/22 | 21:30 | Dunajska Streda vs Steaua Bucuresti | 2.62 | 3.33 | 2.57 |
| 04. 04/08/22 | 03:00 | Juarez FC vs San Luis | 2.52 | 2.92 | 2.97 |
| 05. 04/08/22 | 18:30 | AEK Larnaca vs Partizan | 3.17 | 3.22 | 2.25 |
| 06. 04/08/22 | 19:00 | Stjordals-Blink vs Grorud IL | 2.60 | 3.43 | 2.36 |
| 07. 04/08/22 | 19:00 | Sandnes Ulf vs Sogndal | 2.33 | 3.48 | 2.60 |
| 08. 04/08/22 | 19:30 | Spartak Trnava vs Rakow Czestochowa | 3.02 | 3.33 | 2.28 |
| 09. 04/08/22 | 20:00 | Jonkopings Sodra vs Vasteras SK | 2.40 | 3.57 | 2.76 |
| 10. 04/08/22 | 20:30 | Zorya Lugansk vs Universitatea Craiova | 2.62 | 3.18 | 2.67 |
| 11. 04/08/22 | 21:00 | Sepsi Osk vs Djurgardens IF | 2.58 | 3.24 | 2.68 |
| 12. 04/08/22 | 21:30 | Brondby vs FC Basel | 2.56 | 3.37 | 2.61 |
| 13. 04/08/22 | 22:00 | Hajduk Split vs Vitoria Guimaraes | 2.57 | 3.33 | 2.62 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MANE KUPEWA MAJUKUMU MAPYA BAYERN




**MUNICH, Ujerumani**

MKURUGENZI Mtendaji wa Bayern Munich, Oliver Kahn amefichua kuwa klabu hiyo haina mpango wa kusajili mshambuliaji mwingine baada ya kuondoka kwa Robert Lewandowski.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland, alisaini Barcelona kwa ada ambayo inaweza kufikia euro milioni 50 mapema mwezi huu, na hivyo kumaliza miaka nane ya kukaa na miamba hao wa Bavaria.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, walifanikiwa kumleta Sadio Mane kutoka Liverpool kabla ya Lewandowski kuondoka na Kocha Mkuu, Julian Nagelsmann amefichua kuwa anamwona nyota huyo wa Senegal kama mshambuliaji wa kati.

Nagelsmann amekiri kwamba, anavutiwa na Harry Kane huku kukiwa na mazungumzo kwamba analengwa kuhama msimu ujao - jambo ambalo limemkasirisha Kocha wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte - na Kahn amesema hakuna mshambuliaji mwingine atakayetua hapo Allianz Arena katika dirisha hili la usajili.

"Hatutasajili mshambuliaji mpya. Hakuna majadiliano, hapana," alisema Kahn akiambia Bild.

"Bado tuna chaguo katika timu ya sasa - (Joshua) Zirkzee, (Eric-Maxim) Choupo-Moting na Mathys Tel."

Licha ya kuhusishwa kwa Bayern na Kane, nyota huyo wa England alibainisha hivi karibuni kwamba, ana furaha kuwa Spurs chini ya Conte.

# Firmino hataki kuondoka Liverpool

**LIVERPOOL, England**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Roberto Firmino, amesisitiza kuwa hana nia ya kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto, licha ya kuwapo kwa tetesi kuhusu mustakabali wake.

Firmino atafikisha miaka 31, Oktoba na ameingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Liverpool.

Mbrazil huyo pia aliona muda wake wa kucheza ukiwa mdogo msimu uliopita kutokana na majeraha na sasa ana ushindani ulioongezwa kutoka kwa Darwin Nunez, pamoja na Diogo Jota tayari kuchukua nafasi yake.

Juventus waliripotiwa kutaka kumsajili Firmino na Liverpool wameonyesha nia ya kutaka kumuuza msimu huu wa majira ya joto.

Kocha Jurgen Klopp alinukuliwa akisema wiki iliyopita kuwa "Bobby ni muhimu kwetu."

Na sasa Firmino, ambaye alijiunga na Liverpool kwa ada ya pauni milioni 29 kutoka Hoffenheim mwaka 2015 amesema anataka kubaki.

"Ninaipenda timu hii, Jiji na mashabiki. Niko hapa Liverpool na ninataka kubaki," alisema akiambia TNT Brazil.

Akiwa katika kiwango bora, Firmino alifunga mabao 27 katika mashindano yote msimu wa 2017/18.



## HABARI MICHEZO

301,493/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/22 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.29 | 3.29 | 3.09 |
| 02. 06/08/22 | 17:00 | Bristol City vs Sunderland | 2.21 | 3.24 | 3.29 |
| 03. 06/08/22 | 17:00 | QPR vs Middlesbrough | 2.47 | 3.24 | 2.84 |
| 04. 06/08/22 | 17:00 | Reading vs Cardiff | 2.44 | 3.18 | 2.94 |
| 05. 06/08/22 | 17:00 | Swansea vs Blackburn | 2.36 | 3.19 | 3.04 |
| 06. 06/08/22 | 17:00 | Burton vs Bristol Rovers | 2.39 | 3.33 | 2.88 |
| 07. 06/08/22 | 17:00 | Charlton vs Derby | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 08. 06/08/22 | 17:00 | Exeter vs Port Vale | 2.53 | 3.17 | 2.82 |
| 09. 06/08/22 | 17:00 | Fleetwood Town vs Plymouth | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 10. 06/08/22 | 17:00 | MK Dons vs Sheffield Wed | 2.61 | 3.21 | 2.71 |
| 11. 06/08/22 | 17:00 | Shrewsbury vs Accrington | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 12. 06/08/22 | 17:00 | Barrow vs Bradford City | 2.59 | 3.13 | 2.78 |
| 13. 06/08/22 | 17:00 | Crawley Town vs Leyton Orient | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 14. 06/08/22 | 17:00 | Hartlepool vs AFC Wimbledon | 2.89 | 3.24 | 2.44 |
| 15. 06/08/22 | 17:00 | Mansfield vs Tranmere | 2.26 | 3.19 | 3.24 |
| 16. 06/08/22 | 18:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.73 | 3.23 | 2.53 |
| 17. 06/08/22 | 21:30 | Hansa vs Arminia Bielefeld | 2.64 | 3.34 | 2.59 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 02 - AGOSTI 2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1228 | Sangju Sangmu vs Pohang Steelers | 2.94 | 3.28 | 2.20 |
| 13:00 | 2399 | Mohammedan Sporting Club Dhaka vs Rahmatgonj Mfs | 1.39 | 4.31 | 6.67 |
| 13:00 | 5810 | Shadhinata Krira Sangha vs Sheikh Russel KC | 6.71 | 5.13 | 1.32 |
| 13:30 | 3023 | Jeju Utd vs Seongnam Ilhwa | 1.64 | 3.68 | 4.61 |
| 14:00 | 5478 | Ulsan Hyundai vs FC Seoul | 1.68 | 3.64 | 4.33 |
| 17:00 | 4848 | Kokand 1912 vs Neftchi Fargona | 1.65 | 3.45 | 4.93 |
| 17:00 | 5580 | Deportivo Toluca U20 vs Puebla U20 | 1.97 | 3.48 | 3.28 |
| 17:35 | 4736 | Al Arabi Doha SC vs Qatar SC | 1.73 | 3.53 | 4.22 |
| 18:00 | 2133 | Zalgiris Kaunas vs Suduva | 3.08 | 3.03 | 2.24 |
| 18:00 | 4368 | Lokomotiva Devinska Nova Ves vs Nmsk 1922 Bratislava | 2.00 | 4.03 | 2.85 |
| 18:00 | 4948 | Nasaf Qarshi vs Navbahor Namangan | 1.56 | 3.78 | 5.11 |
| 19:00 | 3077 | HIK Hellerup vs Nykobing FC | 4.02 | 3.73 | 1.72 |
| 19:00 | 3145 | Fremad Amager vs Hillerod | 1.64 | 3.82 | 4.41 |
| 19:30 | 1700 | VfB Eichstatt vs Kickers Wurzburg | 2.74 | 3.53 | 2.21 |
| 19:30 | 2680 | Arab Contractors vs Coca Cola | 3.06 | 3.01 | 2.41 |
| 19:30 | 3429 | FC Liefering vs Vorwarts Steyr | 1.70 | 4.02 | 3.82 |
| 19:30 | 3834 | Ansbach vs TSV Aubstadt | 2.61 | 3.69 | 2.24 |
| 19:30 | 5306 | Nurnberg II vs TSV Rain/Lech | 1.80 | 3.68 | 3.68 |
| 19:45 | 3355 | Al Gharafa SC vs Al-Sailiya SC | 2.11 | 3.57 | 2.89 |
| 20:00 | 1524 | Schweinfurt vs Augsburg II | 1.45 | 4.53 | 5.32 |
| 20:00 | 1659 | Unterhaching vs SV Heimstetten | 1.49 | 4.70 | 5.20 |
| 20:00 | 2467 | Viktoria Aschaffenburg vs Burghausen | 2.29 | 3.65 | 2.70 |
| 20:00 | 2931 | Buchbach vs Illertissen | 2.80 | 3.09 | 2.39 |
| 20:00 | 4909 | Sheriff Tiraspol vs Viktoria Plzen | 2.81 | 2.86 | 2.66 |
| 20:45 | 3538 | Ludogorets Razgrad vs Dinamo Zagreb | 2.79 | 3.04 | 2.54 |
| 21:00 | 2577 | Monaco vs PSV Eindhoven | 2.08 | 3.55 | 3.15 |
| 21:00 | 2858 | KA Akureyri vs KR Reykjavik | 2.17 | 3.39 | 2.90 |
| 21:30 | 1118 | Holyhead Hotspur vs Conwy Borough | 1.90 | 3.59 | 3.39 |
| 21:30 | 2715 | Goytre United vs Cambrian & Clydach Vale | 2.13 | 3.83 | 2.70 |
| 21:30 | 3294 | Prestatyn Town vs Buckley Town | 2.23 | 4.32 | 2.38 |
| 21:30 | 4260 | Llandudno FC vs Holywell Town | 2.11 | 3.63 | 2.85 |
| 21:30 | 4789 | Llanelli AFC vs Cwmbran Celtic | 1.61 | 4.43 | 3.93 |
| 21:30 | 5854 | Taffs Well vs Trefelin FC | 2.01 | 3.43 | 3.23 |
| 21:35 | 5778 | Estudiantes Rio Cuarto vs Deportivo Madryn | 2.38 | 2.84 | 3.04 |
| 21:45 | 3871 | Union Saint Gilloise vs Rangers | 2.66 | 3.27 | 2.51 |
| 21:45 | 5161 | Cambridge Utd vs Millwall | 4.02 | 3.57 | 1.83 |
| 22:00 | 4149 | Benfica vs Midtjylland | 1.24 | 5.58 | 10.96 |
| 22:00 | 5418 | Deportes Recoleta vs CSD Barnechea | 2.70 | 2.95 | 2.70 |

JUMATANO - 03 - AGOSTI 2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:15 | 2052 | Nacional (URU) vs Atletico GO | 1.89 | 3.24 | 3.83 |
| 02:00 | 3144 | Deportivo Cali vs Envigado FC | 1.68 | 3.38 | 4.81 |
| 02:30 | 1282 | NY Red Bulls vs Colorado Rapids | 1.64 | 4.09 | 4.91 |
| 03:10 | 3593 | Defensores Belgrano vs San Martin SJ | 2.28 | 2.84 | 3.24 |
| 03:30 | 1175 | Sport Recife vs Criciuma SC | 2.02 | 3.04 | 3.63 |
| 03:30 | 2502 | Corinthians vs Flamengo | 2.99 | 2.94 | 2.35 |
| 03:30 | 2617 | Deportivo Tachira vs Independiente DV | 2.99 | 3.19 | 2.21 |
| 04:00 | 1652 | Deportivo Toluca vs Puebla FC | 2.23 | 3.33 | 3.07 |
| 04:05 | 2393 | Independiente Santa Fe vs America De Cali | 1.72 | 3.33 | 4.61 |
| 05:00 | 2649 | Seattle Sounders vs FC Dallas | 1.96 | 3.52 | 3.77 |
| 05:05 | 2563 | Dorados vs Club Celaya | 2.43 | 3.00 | 2.81 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MULTICHOICE YAONYA LIGI ZA ULAYA ZIKIREJEA RASMI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu mbalimbali barani Ulaya zikirejea, Kampuni ya MultiChoice Tanzania imetoa onyo kwa wamiliki wa mitandao ya kurusha matangazo kwa njia ya waya (cable), Kampuni za Utangazaji na umma kwa ujumla kuwa hawatosita kuchukua hatua kali na za kisheria kwa yeyote atakayerusha matangazo ya ligi hizo bila idhini yake.

Taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo kwa niaba ya MultiChoice Group, imesema kuwa matangazo hayo yanaruhusiwa kurushwa kupitia Chaneli za SuperSport pekee ambazo hupatikana katika Kisimbuzi cha DStv kinachoendeshwa na MultiChoice Group (MCG).

Imeeleza kampuni hiyo ndiyo ina haki hizo kwa ukanda wote wa Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara na visiwa vya jirani, ikiwamo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Taarifa imeeleza kwa minajiri hiyo, kurusha au kusambaza kwa njia yoyote ile matangazo ya mashindano hayo ya Ligi Kuu mbalimbali ni kinyume cha sheria, kanuni na makubaliano ya haki miliki.

Aidha, imeeleza kuwa Super Sport International (Pty) Limited, ni moja ya kampuni tanzu ndani ya Makampuni ya MaltiChoice inayowakilishwa nchini na MultiChoice Tanzania Limited.

Imezitaja ligi ambazo inahodhi haki ya kurusha matangazo, hivyo ni marufuku kurusha bila idhini yao ni Ligi Kuu ya England, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi ya Europa, Ligi ya Europa Conference, UEFA Super Cup, Kombe la FA England, Kombe la Dunia 2022, mechi ya Ngao ya Jamii, Ligi Kuu Italia, na Ligi Kuu Hispania.




# Kagere, Mugalu, kuagwa kishujaa Simba

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema itawaaga wachezaji wake Meddie Kagera, Chris Mugalu na Thadeo Lwanga kishujaa kutokana na kuitumikia kwa mafanikio makubwa.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema wachezaji hao wanaondoka kwenye klabu hiyo baada ya kutokuwa chaguo la Kocha Mkuu, Zoran Maki, ambaye ameonekana kutoridhishwa na viwango vyao kwa sasa.

"Mugalu, Kegere na Lwanga wapo nchini na sasa wanaongea na uongozi kuona ni kwa namna gani tunasitisha mikataba kwa maslahi ya pande zote mbili. Wamekuwa si chaguo la mwalimu wetu, lakini bado wana mikataba, hivyo wanaendelea na mazungumzo, itakachoamuliwa tutawajulisha," alisema Ahmed.

Alisema iwapo wachezaji hao wataridhia kwa nafsi moja kuondoka, wataandaa utaratibu wa kuwaaga.

"Hawatoondoka hivi hivi, kila mmoja anafahamu mchango mkubwa wa Kagere, Mugalu na Lwanga, tuone ni kwa namna gani wataridhika kwa nafsi moja, na kama haitoshi tutaona ni kwa namna gani tutaandaa namna ya kuwaaga, kwa sababu hawa ni mashujaa wetu," alisema.

Hata hivyo, zipo taarifa kuwa huenda wachezaji hao wakaagwa kwenye Kilele cha Simba Day Agosti 8, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wachezaji hao walikuwa na kikosi hicho nchini Misri ilipokwenda kupiga kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano nchini ya kocha huyo mpya, mwenye uraia wa Ureno na Serbia.

Baada ya mechi ya kirafiki dhidi ya Haras El Haboud, ambapo Simba ilichapwa mabao 2-0, kocha huyo alionyesha kutoridhishwa na viwango vya wachezaji hao.

Kagere, raia wa Rwanda, alisajiliwa na timu hiyo mwaka 2018 akitokea Gor Mahia na kuwa mshindi wa Kiatu cha Dhahabu mara mbili mfululizo, 2019/20 na 2020/21.

Mugalu, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, alisajiliwa 2020 kutoka Lusaka Dynamos ya Zambia, huku Lwanga ambaye ni Mganda, akisajiliwa 2020, akitokea Tanta ya Misri.

Michezo

Jumanne Agosti 2, 2022

Nipashe




## Xavi: Sijui kama De Jong atabaki Barca

UMEFUNIKA...




Jopo la uongozi wa Simba, Mwenyekiti wa Wanachama wa Klabu hiyo, Murtaza Mangungu (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Salim Abdallah 'Try Again' (wa pili kushoto) na Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez (kulia), wakiwa na watendaji wakuu wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, walioshika jezi ya klabu hiyo wakionyesha thamani ya mkataba wa miaka mitano walioingia na Simba kwa kiasi cha Sh. bilioni 26.1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# M-BET YAONYESHA UKUBWA WA SIMBA

## ●●●Yaimwagia Sh. bilioni 26, haijawahi kutokea kwa klabu nchini, yachangia pia usajili shilingi...

**Na Saada Akida**

BAADA ya awali kutangaza kuingia mkataba wa miaka mitano na Kampuni ya M-Bet, huku ikiahidi kuuanika rasmi Agosti Mosi, mwaka huu, hatimaye siku hiyo ilitimia jana kwa Klabu ya Simba na wadhamini wao hao kuweka hadharani thamani ya mkataba huo kuwa ni Sh. bilioni 26.1, ukiwa ni kwa timu ya wakubwa pekee.

Simba imeingia mkataba huo na Kampuni ya M-Bet kuwa wadhamini wao wakuu baada ya kumalizika ule wa awali na SportPesa ambao walidumu nao kwa miaka mitano kwa thamani ya Sh. bilioni nne.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet, Allen Mushi, alisema kampuni hiyo imeingia makubaliano na Simba baada ya kuvutana kwa zaidi ya miezi mitatu.

"M-bet ni kampuni iliyoanzishwa mwaka 2012, tuna miaka 10 hadi sasa tumeamua kuingia kudhamini Simba kutokana na mafanikio yao baada ya kushinda ubingwa wa ligi misimu minne mfululizo.

"Mgawanyo wa fedha utakuwa kama ifuatavyo; mwaka wa kwanza tutatoa Sh. bilioni 4.67, mwaka wa pili billioni 4.92 mwaka wa tatu tutatoa Sh. bilioni 5.2 , mwaka wa nne bilioni 5.51 na mwaka wa tano tutatoa bilioni 5.85," Mushi alisema na kuongeza:

"Simba ni timu kubwa Tanzania na inashika nafasi ya 10 kwenye viwango vya ubora Afrika, kwa nini tusifanye nao kazi." Naye Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema: "Leo [jana] ni siku kubwa kwa Simba na M-Bet, kubwa ni kwa nini M-Bet, kwa sababu kubwa wameanza kukidhi mahitaji yetu.

"Kwa ukubwa wa Simba ni lazima kujihusisha na kampuni ambayo inaongoza kwenye biashara, mkiangalia takwimu M-Bet wanaongoza kwa ukubwa Tanzania.

"Washiriki wote kwa sasa wamejikita kwa Simba tu, hii ni mara ya kwanza kwa mdhamini mkubwa anakuwa na timu kubwa, kwa kuwa huko nyuma mdhamini mkuu alikuwa kwa timu zote, lakini sasa timu zingine tunaweza kutafutia mdhamini wake," Barbara.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alitoa shukrani zake kwa M-Bet kwa udhamini mkubwa na wao wataheshimu mkataba huo huku wakiamini kuwa mdhamini huyo atatekeleza vipengele vya mkataba.

"Fedha hizi zinaenda kutumika katika matumizi yaliyokusudiwa, napenda kutoa shukrani kwa mdhamini aliyepita, amefanya kazi nzuri.

"M-Bet wameonyesha kuwa wako 'siriasi', waliongeza Sh. milioni 400 kwenye usajili wetu mwaka huu," alisema Try Again.

Simba kwa sasa ipo Misri ikijiandaa na msimu mpya, wakati huu ikitarajiwa kurejea nchini Alhamisi wiki hii tayari kwa ajili ya Tamasha la Simba Day litakalofanyika Agosti 8, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Yanga kuivaa Vipers Kilele cha Mwananchi

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

SIKU moja tu baada ya Simba kuja na kaulimbiu ya 'We Are Unstoppable', ikiwa na maana ya 'hatuzuiliki, hatushikiki', wapinzani wao wa jadi, Yanga wamejibu mapigo, baada ya kulipa kwa kaulimbiu 'beauty beauty' kuelekea msimu wa 2022/23 wa mashindano.

Aidha, Yanga imetangaza kukipiga dhidi ya Vipers FC ya Uganda kwenye kilele cha Siku ya Mwananchi, Jumamosi Agosti 6, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizindua Wiki ya Mwananchi' jana, Dar es Salaam, Makamu Rais wa klabu hiyo, Arafat Haji, alisema klabu hiyo inakwenda kuandika historia nyingine kwa kuujaza tena uwanja kuliko hata ilivyokuwa msimu uliopita.

"Natangaza rasmi kuzindua rasmi Wiki ya Mwananchi, tutakuwa na matukio tofauti katika kila pembe zote za Tanzania kuanzia leo hadi Jumamosi ambapo itakuwa kilele chake. Kauli mbiu yetu msimu unaokuja ni kile ambacho tumeshakitekeleza msimu uliopita, yaani 'beauty beauty'. Hiyo ndiyo kauli mbiu yetu na Wanayanga wategemee 'beauty beauty', kwa usajili mzito ambao tumeufanya na utaenda kuakisi hicho tunachokisema kuanzia Agosti 6," alisema Arafat.

Alisema kwenye tamasha hilo, mbali na shamra shamra mbalimbali ambazo zitakuwapo kama kawaida, lakini wamewaalika magwiji maarufu wa mpira barani Afrika ambao watafika kushuhudia tamasha hilo, lakini waandishi wa habari kutoka ndani na nje ya Bara la Afrika pia watakuwapo.

"Mwaka jana tuliujaza uwanja tukaweka historia, mwaka huu tukaivunja historia yetu wenyewe na Wanayanga huwa hatushindwi kitu tukiamua, kama tuliweza kushangaza dunia kwenye mapokezi ya ubingwa wetu, hili hatuwezi kushindwa. Kwenye kilele chetu tunakwenda kucheza na timu bingwa mwenzetu, bingwa hadhi yake kucheza na bingwa mwenzake, kwa hiyo tunacheza na Mabingwa wa Uganda, Vipers FC," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >